epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Nipashe

Alhamisi Novemba 21, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581867

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA WA 22

**GUARDIOLA AONGEZA MWAKA MMOJA CITY**

UKURASA WA 5

KUCHOMA MKE KWA MAGUNIA YA MKAA

**MSHTAKIWA ADAI ALITOA TAARIFA YA UONGO POLISI KIFO CHA MKEWE**

MFANYABIASHARA Khamis Lu-wongo (38) amedai mahakamani...

UKURASA WA 19

**MJUKUU ADAIWA KUMUUA BIBI KWA NYUNDO NA JIWE**

MTU anayedhaniwa kuwa na tatizo la afya ya akili, Ronald Ulomi...

UKURASA WA 19

**TGNP YAONYA UKATILI WA KIJINSIA UCHAGUZI SERIKALI ZA MITAA**

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TGNP), umetoa tahadhari kuhusu...

**Kumekucha, kishindo cha uzinduzi kampeni za vyama kila kona**

UKURASA 3

SAMIA ASISITIZA...

# Tutabomoa Kariakoo

• **Arejea** nchini akifikia eneo la jengo lililoporomoka, asema vibali vya ujenzi vilitoka bila... *Endelea ukurasa 2*




Rais Samia Suluhu Hassan akipata maelezo kutoka kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alipokagua eneo la maafa ya ajali ya kuporomoka kwa ghorofa Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**



# Wastaafu walipwa mapunjo ya mafao

UKURASA 2

**MICHEZO** RAMOVIC WA YANGA AWAVURUGA AL HILAL UK.24 **KATUNI** UK.6



Mafundi wakishusha vitendea kazi katika ujenzi unaoendelea wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka kwenye Barabara ya Bagamoyo, eneo la Afrikana, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

## SAMIA ASISITIZA...

# Tutabomoa Kariakoo

**Na Halfani Chusi**

RAIS Samia Suluhu Hassan amerejea nchini akitokea Brazil na kwenda moja kwa moja Kariakoo, jijini Dar es Salaam kuwafariji wafanyabiashara na wananchi kufuatia tukio la kuporomoka kwa jengo kulikosababisha vifo vya watu 20 na makumi wengine kujeruhiwa.

Vilevile, Mkuu wa Nchi amesema kuwa baada ya kutembelea eneo la tukio, amebaini kulikuwa na "shida katika usimamizi wa ujenzi wa jengo hilo", akitaja maeneo mawili mahususi nondo na kuta hazikuwa na ubora.

Akizungumza na wananchi baada ya kutembelea eneo la tukio, Rais Samia alisema kuwa watu waliofariki dunia kutokana na tukio hilo lililotokea Jumamosi asubuhi, ilikuwa 20 kufikia jana saa tatu asubuhi.

Rais alielekeza maduka ambayo yako mbali na eneo la tukio, yafunguliwe ili wafanyabiashara waendelee na kazi na kueleza kuwa majeruhi wanaopatiwa matibabu, wamebaki watatu na hali zao zinaendelea kuimarika.

Alisema jengo hilo limeporomoka kwa kuwa ujenzi wake hausimamiwa vizuri, kwamba hata kwa macho ya kawaida, linaonekana ujenzi wake haukuzingatia viwango stahiki.

Rais Samia aliyekuwa anazungumza kwa hisia za huzuni, alisema jitihada za serikali zililenga kuwaokoa wote walionaswa katika ajali hiyo wakiwa hai lakini isivyo bahati wengine imeshindikana. Alisema tukio hilo limegusa hisia za wengi na si msiba wa wafiwa pekee, bali wa taifa zima.

"Tumeguswa na tukio hili, hata wenzetu waliokolewa bila shaka hawako sawa, lakini Mungu ana kazi nao, wajipe moyo na waendelee na shughuli zao kama kawaida," alisema.

Rais Samia alisema alipokea taarifa za tukio hilo akiwa Brazil alikoalikwa kushiriki "mkutano wa wakubwa wa dunia" -- G20, akatoa maelekezo na jana alikwenda kushuhudia hali ilivyokuwa na kubainisha kwamba janga lilikuwa kubwa.

"Maelekezo niliyopata nimeona hali na umoja wa watanzania katika majanga haya, janga hili kwangu tangu niingie madarakani kwa ukubwa ni la tatu.

"Lakini katika majanga yote tumeona watanzania wanavyojitoa kusaidia, kazi imefanyika kwa bidii na weledi mkubwa kunusuru watanzania wenzetu.

"Tukio hili limetupa ujumbe mkubwa wa kuangalia usalama wa majengo yetu Kariakoo. Wakati ninaonyeshwa, ukiliangalia lilivyojengwa, kuta zake na nondo, halikusimamiwa vizuri," alisisitiza Rais Samia.

Alisema tukio hilo ni somo kwa serikali na mpango uliopo kupitia tume iliyoundwa ni kuingia Kariakoo kuangalia ubora wa majengo mengine.

Rais pia aliwapongeza wananchi kwa kutokukimbilia kuchukua mali za wafanyabiashara baada ya janga hilo na kujikita katika uokoaji.

Alisema mali zote zilizopo ndani ya jengo hilo zitahifadhiwa mahali salama na kisha baadaye wataitwa wahusika kwa ajili ya kuzitambua.

Rais Samia alisema taarifa itakayotolewa na timu iliyoundwa baada ya kukagua majengo, wataiweka bayana na kama itashauri kubomoa baadhi ya majengo yatabomolewa.

Alisema kuwa hata taarifa za tume iliyoundwa mwaka 2003 kwa kazi kama hiyo, zitajumuishwa na za timu mpya iliyoundwa na kufanyia kazi ushauri wa tume zote.

Pia aliwataka watendaji wa serikali na mtu mmoja mmoja kutimiza wajibu wake, akitolea mfano wa jengo lililoporomoka lilijengwa kwa vibali, lakini hakukuwa na usimamizi mzuri katika kutazama ubora wake.

### ATEMBELEA MUHIMBILI

Akiwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Rais Samia alitembelea baadhi ya wodi walimolazwa majeruhi wa ajali hiyo.

Akizungumza na baadhi ya wagonjwa hao, Rais Samia aliwapa pole na kuwataka wasikate tamaa kwa kuwa watapona na kurejea katika hali zao za awali. Katika moja ya wodi, Rais Samia alimjulia hali mmoja wa waathirika wa tukio hilo aitwaye Jonas. Sehemu ya mazungumzo yao ilikuwa hivi:

**Rais Samia:** "Unaendeleaje Jonas, Pole! Ulikuwa unafanya nini Kariakoo?

**Jonas:** Nilikuwa ninamsaidia baba kuuza duka.

**Rais Samia:** Ulikuwa dukani kumsaidia baba, Mungu amekusaidia, Inshallah utapona! Madaktari wanawatibia, usijali utapona, ugua pole Jonas!

**Jonas:** Asante Mheshimiwa Rais!

Mmoja wa manusura waliokuwa Muhimbili jana, alisema ni mtahiniwa wa Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne na alikuwa amefanya mitihani saba, alipaswa kufanya mtihani wa mwisho juma hili, lakini hajaufanya.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms/WhatsApp: +255 677 020 701 Email: costomerrelations@guardian.co.tz***


## KUMBUKUMBU



**ROSE SIMON IVAMBI**

Leo tarehe **21/11/2024** , Mama yetu mpendwa **Rose Simon Ivambi** umetimiza miaka 15 tangu utwaliwe na Mungu Baba kutoka Dunia hii. Sisi wanao **Frida, Janeth,Veronica na Sebastian** pamoja na wajukuu wako wote na vitukuu, tunaendelea kukuombea kwa Mungu akujalie pumziko la amani. Kamwe hatutasahau mema yote uliyotutendea wakati wa uhai wako Tunaomba Mwenyezi Mungu ayapokee mema yako na kukukaribisha katika utukufu wake.

**Bwana alitoa na Bwana ametwaa. Jina lake lihimidiwe.**

Amina.


# Wastaafu walipwa mapunjo ya mafao

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Ridhiwani Kikwete, amesema hadi jana, wastaafu 10,414 waliokoma utumishi kuanzia Julai 2022 na kulipwa mafao kwa kikokotoo cha zamani, wamelipwa mapunjo kulingana na kikokotoo kipya.

Aidha, wastaafu wapya 2,479 wa kuanzia Julai 1, mwaka huu, wameshalipwa mafao kwa kutumia kikokotoo kipya kilichoboreshwa na kazi bado inaendelea kwa kutekeleza maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza jana wakati wa semina kwa wastaafu watarajiwa wa Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Kikwete alisema serikali ilisikia kilio cha wastaafu na kupitia hotuba ya bajeti ya mwaka 2024/25 iliyosomwa Juni, mwaka huu, serikali ilitangaza kuboreshwa kwa mafao hayo kwa kutumia kikokotoo kipya.

Kikokotoo cha awali kilikuwa asilimia 25 kwa mifuko yote ya PSSSF na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) lakini baada ya malalamiko, kilipandishwa hadi asilimia 33. Julai, mwaka huu serikali ilitangaza kikokotoo kipya cha asilimia 40 kwa wastaafu wa PSSSF na asilimia 35 kwa wastaafu wa NSSF, hatua ambayo itaweka vikokotoo viwili.

Mwaka 2018, Nipashe ilichapisha habari iliyoibua hisia kitaifa kuhusu kanuni ya kikokotoo ambayo iliweka usawa wa asilimia 25 kwa wastaafu wote baada ya kuunganisha Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF), Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma (PSPF), Mfuko wa Akiba wa Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (LAPF) na Mfuko wa Pensheni wa Wafanyakazi wa Serikali (GEPF) na kuunda PSSSF huku NSSF ikibaki kama awali.

Jana, Waziri Kikwete alisema hatua zingine zilizochukuliwa ni kuboresha maslahi ya wastaafu ambao wengi wamekuwa wakipokea kima cha chini cha Sh. 100,000 na kuanzia pensheni ya Januari, 2025 pensheni yao ya mwezi itaongezeka hadi kufikia Sh. 150,000.

Aidha, alisema wastaafu ambao walikuwa wanapokea pensheni ambayo ni zaidi ya Sh. 150,000.00 na watapewa ongezeka la asilimia mbili kila mmoja, huku mstaafu yeyote anayepokea pensheni ya PSSSF akifariki dunia, mfuko utatoa Sh. 500,000 kwa ajili ya maziko.

Pia alisema mstaafu yeyote akifariki dunia, wategemezi wake wanaotambulika na sheria ya mfuko watalipwa mkupuo wa miezi 36 wa pensheni ya mwezi ya mstaafu husika.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Abdul-Razaq Badru, alisema mwaka jana walifanya semina kwa waajiri 746 na mwaka huu watawafikia 878 kwa ajili ya kuimarisha utoaji huduma za wanachama eneo la penseni.

"Moja ya mafao mengi tunayolipa ni pensheni. Jumla mafao yaliyolipwa tangu kuanza mfuko ni Sh. trilioni 10.46 na wanufaika ni 310,458 na kwamba mwaka huu wa fedha, watalipa mafao ya uzeeni na mengineyo wastaafu 11,622 ya jumla ya Sh. bilioni 560. Kwa mwaka huu, mafao yatafikia tathimini ya Sh. trilioni 1.5," alisema.

Pia alisema mfuko unaendelea kuimarika na unaendelea kutimiza jukumu lake la kulipa mafao, likiwamo fao la uzeeni.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms/WhatsApp: +255 677 020 701***

***Email:costomerrelations@guardian.co.tz***

# Kishindo kampeni uchaguzi S/Mitaa

**Na Waandishi Wetu**

KIVUMBI cha uzinduzi wa kampeni za uchaguzi wa serikali za mitaa kilianza rasmi jana katika maeneo mbalimbali kwa viongozi wa vyama vitatu vya siasa ambao wametawanyika kila kona.

Vyama hivyo ni Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Chama Cha Mapinduzi (CCM) na ACT-Wazalendo.

Katika kampeni hizo, CCM ilizindua kwa viongozi na makada wakiwa katika mikoa tofauti huku CHADEMA ikifungua pazia kwa Makamu Mwenyekiti kufanya hivyo Ikungi mkoani Singida.

Aidha, viongozi wengine wa chama hicho watakuwa katika maeneo mbalimbali kuanzia leo huku Mwenyekiti wake, Freeman Mbowe, akitazamiwa leo kufufua kampeni leo mkoani Mbeya.

### CCM NA 4R

CCM katika kampeni zake imejivunia kutumia falsafa ya 4R ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kufanya kampeni hizo kistaarabu na haihitaji kufanya kejeli wala matusi.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Amos Makalla, alisema jana mkoani Dar es Salaam kuwa kampeni zitafanyika kistaarabu kwa sababu ni chama tawala kinachoongoza, hivyo kina ajenda na hoja nyingi za kushawishi Watanzania waichague.

Akizindua kampeni hizo kwa mkoa wa Dar es Salaam akiwa Temeke, Makalla alisema: "Mtu ambaye hana hoja ataendelea kutukana na kutoa vitisho, sisi tutawajibu kwa kampeni za hoja ili wananchi wapime wenyewe nani anapaswa kupewa kura.

Makalla aliagiza kampeni ya mtaa kwa mtaa, nyumba kwa nyumba, kitanda kwa kitanda, mtu kwa mtu ifanywe ili CCM ishinde.

Naye Mlezi wa CCM Mkoa wa Katavi na Naibu Katibu Mkuu wa Chama Zanzibar, Dk. Mohamed Said Dimwa, amelisihi wananchi wa mkoa huo bila kujali tofauti za kisiasa, kidini na kikabila, kuweka mbele maslahi ya maendeleo yao kwa kuwachagua wagombea wote wa chama hicho.

Akizungumza katika Kijiji cha Ikola A, Dk. Dimwa alisema ushindi kwa CCM katika uchaguzi huo una tija na manufaa makubwa kwa wananchi wote si kwa wanachama wa CCM pekee kwa kuwa fursa za maendeleo zinapatikana kutokana na mipango mizuri ya viongozi wanaotokana na chama hicho. Kwa mujibu wa Dimwa, wagombea wote wa CCM watakaoshinda, watakuwa na kazi ya kuendeleza mikakati ya maendeleo iliyoachwa na viongozi waliomaliza muda wao ambao wamefanya mambo makubwa.

Dk. Dimwa pia alisema CCM imeendelea kuwa chama kiongozi katika ubobezi wa kisiasa hasa katika kutekeleza kwa vitendo ahadi zake kupitia utekelezaji wa ilani ya CCM ya mwaka 2020 -2025 kwa manufaa ya wananchi wote mijini na vijijini katika maeneo yote ya mkoa wa Katavi.

"Wito wangu kwenu wananchi nyote katika kata zote 58 zilizoko katika mkoa huu, jitokezeni Novemba 27, 2024 mkawapigie kura nyingi wagombea wote wa CCM ili wakatekeleze mahitaji yenu kwa vitendo," alisema.

Naye Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Katavi, Idd Kimanta, alisema CCM imejipanga vizuri kuhakikisha wagombea wote wa chama hicho wanashinda katika maeneo yao.

### WATAKAOSHINDA WAONYWA

Mkoani Dodoma, CCM imewataka wagombea watakaoshinda uchaguzi wa serikali za mitaa kutovimba kama maharagwe na kutanguliza maslahi binafsi kwa kuwa haitasita kuwaondoa katikati ya muhula wa uongozi.

Pia imeonya kuwa diwani atakayepoteza mtaa kwenye uchaguzi huo, atatakiwa kujitafakari kabla ya kugombea uchaguzi mkuu ujao.

Akizindua kampeni mkoani hapa kwa niaba ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango ambaye ni Mlezi wa Dodoma, Mwenyekiti wa CCM Mkoa huo, Adam Kimbisa, alisema wagombea wa nafasi za wenyeviti wa vijiji, mitaa na vitongoji hawapaswi kujigeuza kuwa miungu watu baada ya kuchaguliwa bali wahakikishe wanawahudumia wananchi na kusaidia kukivusha chama kwenye uchaguzi mkuu.

### 'PASSWORD' YA CCM

Katibu wa Halmashauri Kuu, Siasa na Uhusiano wa Kimataifa (SUKI) ya CCM, Rabia Hamid, alisema vyama vya upinzani visitegemee mbinu iliyotumika katika uchaguzi wa serikali za mitaa kuwapiku kisiasa, itatumika kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Rabia ambaye ni mlezi wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, alisema wakati akizindua kampeni hizo kwenye viwanja vya Pasua Sokoni, Manispaa ya Moshi kuwa hizo ni salamu kwa wapinzani kwamba atambue CCM inatambua umuhimu wa kuweka serikali za mitaa madarakani. Alisema viongozi wa mitaa ni watu muhimu wanaokaa na wananchi na kuwataka kutotabiri kuwa mbinu inayotumika sasa itatumika tena mwakani.

### CHADEMA MOTO

Baada ya Lissu kuzindua rasmi kampeni hizo jana. CHADEMA inatarajiwa kuonesha makala yake zaidi leo wakati Mbowe akiwa Mbeya na Lissu atakuwa Tarime mkoani Mara.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa Chama hicho, John Mrema, Naibu Katibu wa CHADEMA Zanzibar, Salum Mwalimu, atakuwa Bunda Mjini.

Aidha, Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema, atanguruma Kilombero mkoani Morogoro na Lucas Ngoto atakuwa Tarime.

### ACT KIGOMA, PWANI

Viongozi waandamizi wa Chama cha ACT-Wazalendo, wametawanyika katika maeneo mbalimbali kunadi wagombea wake, kuanzia jana.

Ofisa Habari wa ACT-Wazalendo, Abdallah Hamisi, alisema jana kuwa kiongozi wa chama hicho, Dorothy Semu, ataendesha kampeni mkoani Pwani wakati kiongozi mstaafu, Zitto Kabwe, atapiga kambi Kigoma.

"Viongozi wetu wote pamoja na wajumbe wa Kamati Kuu wametawanyika maeneo mbalimbali. Makamu Mwenyekiti, Isihaka Mchinjita, atakuwa Morogoro, Naibu Katibu Mkuu (Bara), Ester Thomas yuko Mwanza na Ismail Jussa yuko Tanga," alisema.

Alisema Mwenyekiti mstaafu wa chama hicho, Juma Duni Haji, atanadi wagombea wa Dar es Salaam wakati Katibu Mkuu wa chama, Ado Shaibu, atakuwa Tunduru.

**Imeandikwa na Romana Mallya, Elizabeth Zaya, Restuta James (Dar), Marry Mosha (Moshi) na Augusta Njoji (Dodoma)**

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms/WhatsApp: +255 677 020 701***
***Email:costomerrelations@guardian.co.tz***

# HakiElimu yataka usawa kwa shule za Kiswahili, Kiingereza

**Elizabeth Zaya na Grace Mwakalinga**

TAASISI ya HakiElimu Tanzania, imeomba serikali kutengeneza mazingira ya usawa kwa shule za msingi za umma zenye mchepuo wa Kiingereza na Kiswahili.

Kadhalika, imehoji sababu za shule hizo kutoza ada kwa madai kuwa kufanya hivyo ni kinyume cha Sera ya Elimu ambayo inazitaka shule za umma kutoa elimu bure.

HakiElimu pia imehoji sababu za shule za mchepuo wa Kiingereza kupewa hadhi ya juu huku zenye mchepuo wa Kiswahili zikishushwa hadhi.

Taasisi hiyo ambayo imekuwa ikijihusisha na masuala ya elimu kwa muda mrefu, imehoji sababu ya shule hizo za Kiingereza za umma kupewa kipaumbele zaidi kwa kuboreshewa mazingira ya kujifunzia na kufundishia kuliko shule za mchepuo wa Kiswahili.

"Kwa bahati mbaya kumekuwa na kasumba ya kuamini kuwa shule za umma za mchepuo wa Kiingereza zina hadhi kuliko za umma za mchepuo wa Kiswahili. Dhana hii inazidi kuota mzizi na kusambaa kwa watu wengi na kusababisha matabaka ndani ya mfumo wa elimu," alisema Mkurugenzi Mtendaji wa HakiElimu, Dk. John Kalage, wakati akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana.

"Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023 inaeleza kuwa lugha ya kufundishia kwa elimu ya msingi ni Kiswahili isipokuwa kwa ambazo zitaomba na kukubaliwa kufundisha kwa Kiingereza kwa mujibu wa sera hiyo," alibainisha.

Dk. Kalage alisema lugha zote mbili zinabeba hadhi sawa katika utoaji wa elimu nchini na si kweli kwamba kwa shule za mchepuo wa Kiingereza zinakuwa na hadhi zaidi ya zile za mchepuo wa Kiswahili.

Kuhusu utozaji ada kwa shule za mchepuo wa Kiingereza, Dk. Kalage alisema shule hizo zinafanya hivyo kinyume cha sera ya utoaji elimu msingi bila ada.

"Kwa mujibu wa uchambuzi wetu, watoto hulipa kati ya Sh. 300,000 na 600,000 kiwango ambacho kinasababisha wazazi wenye kipato duni kuwahamishia watoto kwenye shule za mchepuo wa Kiswahili. Kwa nini shule za umma za mchepuo wa Kiingereza zinakiuka sera ya elimu ambayo inazitaka shule za umma kutokutoza ada?" alihoji.

Dk. Kalage alitolea mfano wa ufafanuzi uliotolewa hivi karibuni na Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Hassan Bomboko, kuhusiana na Shule ya Msingi Ubungo National Housing iliyodaiwa kwamba imeuzwa.


"HakiElimu inapongeza uongozi wa wilaya ya Ubungo kujitokeza haraka kutoa ufafanuzi juu ya taharuki hiyo, lakini tumeshitushwa na kauli ya uongozi huo kwamba shule hiyo inapandishwa hadhi kuwa shule ya umma ya mchepuo wa Kiingereza, alisema.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms/WhatsApp: +255 677 020 701***



Skani hapa kutembelea chaneli yetu

# UONGOZI BENKI UBA WATEMBELEA THE GUARDIAN LTD




Ofisa Mtendaji Mkuu na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya UBA Afrika, Gbenga Makinde (katikati mwenye miwani), akiwa pamoja na Naibu Meneja Mkuu wa Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Jackson Paulo (kushoto kwake), pamoja na wakuu wa idara mbalimbali za TGL na benki hiyo, baada ya kuwasili katika ofisi za kampuni hiyo, Mikocheni, Dar es Salaam jana kwa ziara ya kikazi. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Ofisa Mtendaji Mkuu na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya UBA Afrika, Gbenga Makinde (wa tatu kulia) na ujumbe wake, wakipata maelezo kutoka kwa Ofisa Mwandamizi wa Matangazo wa TGL, Eliupendo Lema (katikati). Kushoto ni Meneja wa Fedha wa TGL, Samuel Orgeness na Naibu Meneja Mkuu, Jackson Paulo.



Naibu Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Epson Luhwago (wa tatu kulia), akitoa maelezo kwa Ofisa Mtendaji Mkuu na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya UBA Afrika, Gbenga Makinde, kuhusu uzalishaji wa habari, alipotembelea chumba cha habari cha TGL. Kulia ni Mhariri Mtendaji wa Nipashe, Beatrice Bandawe na (kushoto) ni Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa Benki hiyo, Nobert Kabendela.



Meneja wa Kiwanda cha Uchapishaji cha TGL, Balasubramaniyan Venkadachalam (kulia), akitoa maelezo kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki hiyo, Gbenga Makinde na ujumbe wake, kuhusu uzalishaji wa magazeti.



Naibu Meneja Mkuu wa TGL, Jackson Paulo (kulia), akifurahia jambo na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki hiyo, Gbenga Makinde. Kushoto ni Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa Benki hiyo, Nobert Kabendela.

KESI KUCHOMA MKE KWA MAGUNIA

# Mshtakiwa niliwadanganya polisi kifo cha mke wangu

**Na Grace Gurisha**

MFANYABIASHARA Khamis Luwongo (38) amedai mahakamani kuwa alilidanganya Jeshi la Polisi kwamba alimuua na kuchoma moto mwili wa mke wake Naomi Marijani kutokana na mateso aliyokuwa akiyapata, hivyo ameomba aachwe huru akamtafute kwa kuwa yupo hai.

Pia amedai kuwa upande wa Jamhuri pamoja na Mkemia Mkuu wa Serikali wameshindwa kuthibitisha kwamba aliyefariki dunia ni Naomi kwa sababu hakuna majibu ya vinasaba (DNA) yaliyoonesha hivyo katika ripoti iliyoletwa na shahidi.

Luwongo alidai hayo hayo juzi mbele ya Jaji Hamidu Mwanga wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam huku akiongozwa na Wakili wake, Hilda Mushi wakati anatoa utetezi wake katika kesi ya mauji ya mke wake inayomkabili.

Alidai kuwa mawakili wa serikali wanataka ahukumiwe kunyongwa, akihoji "vipi nikihukumiwa kunyongwa halafu baadaye mke wangu akatokea?"

Alidai, "Mke wangu hajafa kwa sababu nilichokichoma ni mabaki ya mwili uliokuwamo katika kaburi ndani ya shamba nililonunua mkoani Morogoro pamoja na mabaki ya mzoga, ndiyo maana hata ripoti ya Mkemia haijaonesha kama mabaki hayo ni ya Naomi," alidai Luwongo.

Mshtakiwa huyo alidai kuwa askari polisi na ndugu wa marehemu walikuwa wanataka maiti, akawaza atawonesha maiti gani ili aepuke mateso hayo, akawaza awapeleke sehemu yoyote yenye makaburi, akakumbuka kwenye shamba lake lililoko Morogoro.

"Nililinunua kwa ajili ya kuanzisha kilimo cha kisiasa, nililifyeka nikataka kujenga nyumba ya wafanyakazi, nikachimba mashimo matano kwa ajili ya kupanda migomba ya kisasa na shimo kwa ajili ya choo," alidai mshtakiwa Luwongo.

Alidai kuwa yale majani yaliyokuwa yamefyekwa na kijana wake, walipokwenda kuyazoa wakakuta mifupa ya mzoga wa mnyama, akamwambia kijana wake akauchukue.

"Kuna eneo lingine nililokuwa nimelinunua, kulikuwa na kaburi lakini tukakubaliana na wenye eneo hilo wakalihamishe na mimi nikaanza ujenzi ili nihamie na familia yangu, lakini ule msingi ulipoharibika, nikawaambia wale vijana wachimbe udongo kwa ajili ya kufukia," alidai.

Luwongo alidai baada ya kuchimba, wakaanza kutoa mifupa akaona hao waliohamisha lile kaburi hawakuteleleza kazi yao vizuri na kwamba hiyo mifupa ni ya marehemu waliyehamisha mwili wake.

Alidai kuwa siku hiyo alikuwa na safari ya kwenda kwenye shamba la Morogoro, hivyo aliichukua mifupa hiyo akaipeleka huko kuirundika kama uchafu, na akawaambia vijana wachome moto.

"Kwa kuwa ninajua kuwa majivu ni mbolea, nikayachukua yale majivu nikapandia migomba," alidai Luwongo.

Alidai kuwa Julai 15, 2019, alipelekwa Kituo Kikuu cha Polisi mkoani Dar es Salaam ambako aliwakuta ndugu wa mkewe, alipelekwa kwa Mkuu wa Upelelezi Camilius Wambura wakati huo, aliwakuta maofisa wengi wakubwa wa Polisi.

Alidai kuwa Kamanda Wambura alimwuliza "maiti ya mkeo iko wapi?" Kwa sababu meseji zote hizo amejitumia mwenyewe kulidanganya Jeshi la Polisi lakini yeye akasema hajui na taarifa za mkewe amefungua jalada polisi.

"Mkuu wa Upelelezi akaniambia 'sasa sisi kama Jeshi la Polisi tutakuelekeza namna maiti ya mkeo iliko'. Baada ya hapo nilivuliwa nguo zote, nikabaki uchi, nikafungwa kamba, nikaning'inizwa kwenye mabomba kichwa chini miguu juu na mwingine akawa anampiga kwenye unyayo," alidai.

Mshtakiwa huyo alidai kuwa aliomba wamwache apumzike, akiahidi kuwaambia ukweli, hivyo walimwachia na baadye wakampeleka mahabusu. Alidai kuwa kutokana na mateso yale aliyokuwa akiyapata polisi, alikumbuka yale majivu, akaona awapeleke shambani.

"Kwahiyo, ili kujiokoa na mateso hayo, nikawaambia 'hapo ndipo alipo mke wangu'. Siku hiyo, saa 10 usiku, askari wale waliniamsha niwapeleke ndipo nikaamua kutunga stori ya uongo, lakini si kweli! Kwanza, hata huo mkaa wanasema magunia mawili si kweli.

"Mashahidi wanaozungumzia huu mkaa ni kijana wangu ambaye alisema alileta viroba viwili akaviweka kwenye gari, lakini shahidi mwingine alisema alileta kiroba kimoja cha mkaa, hakuna magunia mawili ya mkaa, ni kiroba kimoja," alidai.

Alidai kuwa baada ya mkewe kutoonekana, walitumia mkaa huo kupika hadi ukaisha na mkaa mwingine aliwasha gari akaupeleka kwa mwanamke mwingine.

Akizungumzia matone ya damu yaliyokutwa pembeni mwa kitanda, chaga na ukutani alidai inawezekana ni damu za hedhi kwa kuwa alikuwa ana tabia za kuingiza wanawake katika chumba chake na pia inaweza ikawa hata damu ya mtoto wake wa kike, anaweza akawa amejikata.

"Na ndiyo maana kwenye ripoti ya Mkemia imeonesha kwamba damu hiyo ni ya jinsia ya kike. Hata mke wangu alikuwa anaingia katika siku zake kwa sababu na yeye ni mwanamke na pia hivi sina akili kiasi miezi miwili niache kufuta matone hayo ya damu," alidai

Mshtakiwa Luwonga ambaye ni mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam, anadaiwa kuwa Mei 15, 2019, akiwa Gezaulole , wilayani Kigamboni, alimuua Naomi Marijani kisha kuchoma moto mwili wake, akitumia magunia ya mkaa.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**INATANGAZWA TENA: MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA: MPANGO WA UREJESHAJI STAHILI ZA WAGUSWA WA BOMBA LA MAFUTA - UTEKELEZAJI WA MPANGO WA KUENDELEZA UFUGAJI BORA WA WANYAMA. KUMBUKUMBU NA.: 00000619**

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD ("EACOP LTD") inaalika kampuni au mashirika yenye uzoefu na sifa nzuri kuleta maombi yakuonyesha nia yao ya kubuni na kutekeleza Mpango wa ufugaji bora wa Wanyama kwa kaya zilizoathiriwa na mradi wa EACOP.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la chini ya ardhi linalovuka mipaka kwa ajili ya kusafirisha mafuta ghafi kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda hadi pwani ya mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kuuza kwenye masoko ya kimataifa. Bomba hilo litaanzia Kabaale, Wilaya ya Hoima nchini Uganda hadi rasi ya Chongoleani mkoani Tanga, Tanzania, likipitia katika mikoa nane – Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga, halmashauri za wilaya 27 na vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA HUDUMA:**

EACOP inatekeleza mipango ya urejeshaji wa maisha kwa kaya zilizoathiriwa na Mradi. EACOP iko mbioni kuanza utekelezaji wa Mpango wa kuendeleza ufugaji bora wa Wanyama kwa waguswa katika mikoa minne ambako utekelezaji wa mradi wa EACOP unafanyika. Uandaaji wa mpango huu uko katika hatua za mwisho na huenda ukajumuisha lakini hauishii katika:

- Ushirikishwaji wa kaya ili kuthibitisha uwezo wao wa kuwa sehemu ya mpango.
- Uainishaji wa kaya kulingana na miundo tofauti ya mpango.
- Mafunzo na kuzijengea kaya uwezo katikamasuala yote muhimu katika uzalishaji na usimamizi bora wa mifugo na wanyama wadogo wadogo wa kufugwa.
- Mafunzo kwa watoa huduma za ughani za mifugo katika jamii.
- Kuandaa na kutoa mafunzo juu ya kalenda za usimamizi wa mifugo.
- Kusaidia kuanzisha vituo vya wafugaji wa mifugo.
- Kusaidia uanzishaji na uendelezaji wa vyama au ushirika wa wafugaji.
- Kukarabati mabwawa ya kuogesha mifugo.
- Kuunganisha kaya zilizoathiriwa na Mradi (PAHs) na sekta binafsi kwa ajili ya kupata mbegu bora za mifugo kwa kukodisha ng'ombe wa nyama na maziwa.
- Kutoa ushauri na kusaidia upatikanaji wa fursa za kuongeza thamani ya mazao ya mifugo.
- Kutoa huduma za ughani kwa kaya za waguswa kwa kipindi cha miezi 18-24.

**VIGEZO MUHIMU:**

**Mashirika yenye nia yanaalikwa kuandika ombi lao na:**

- Maelezo ya miradi sawa au shughuli zilizofanywa, ambazo zinatoa ushahidi wa timu yenye sifa na inayopatikana, uzoefu kwenye mikoa inayopitiwa na mradi wa Bomba, na rekodi ya kufuatilia ya uzoefu ulioorodheshwa hapo juu.
- Uthibitisho wa usajili na Asasi husika za Usajili Tanzania (BRELA, NGO Registration, OSHA)
- Uthibitisho wa usajili na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha kuidhinisha Kodi kwa mwaka wa hivi karibuni unaopatikana.
- Muonyesha nia awe amekwisha jisajili au amekwisha tuma maombi yaliyoidhinishwa kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani.
- Uthibitisho wa taarifa za Ukaguzi wa hesabu wa kampuni za hivi karibuni.
- Ushahidi wa mfumo wa Usimamizi wa Ubora, Afya, Usalama, na Mazingira (QHSE), shirika, na mchakato kwa kufuata viwango vya Serikali na Viwanda vinavyotumika kwa kazi sawa.
- Uthibitisho wa sera za kupambana na rushwa, kupambana na kutoa hongo, kuzingatia sheria na haki za binadamu.

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **11:00** jioni Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **1/12/2024**. Kichwa cha Barua Pepe kiwe: **EOI 00000619 Mpango wa ufugaji bora wa Wanyama**. Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20. **Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.**

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yaliyoonesha nia kulingana na Tangazo hili la Nia ya kutoa Huduma, na kisha kufanya tathmini kulingana na vigezo vya ndani vya EACOP ili kubaini makampuni yenye sifa yatakayojumuishwa kwenye orodha ya awali ya makampuni yenye vigezo. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD ina haki ya kuteua au kukataa kampuni na kubaki na maamuzi yake bila ya kutoa sababu kwa kamapuni husika.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kasi kuhusu matumizi sahihi ya vyoo inapaswa kuongezwa

**NOVEMBA** 19 kila mwaka hufanyika maadhimisho ya Siku ya Choo Duniani. Kaulimbiu ya mwaka huu ilikuwa kuongeza kasi ya mabadiliko katika upatikanaji wa majisafi na usafi wa mazingira. Yote hiyo ni katika kutekeleza lengo la sita la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG).

Tanzania ikiwa mwanachama wa Umoja wa Mataifa, iliungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha siku hiyo kwa lengo la kuhamasisha jamii kuwa na vyoo bora pamoja na matumizi sahihi ya huduma ya choo. Siku hiyo huadhimishwa kwa ajili ya kuhamasisha na kutoa elimu ya afya hasa katika matumizi ya vyoo kwa usafi wa mazingira na afya kwa ujumla.

Matumizi sahihi ya vyoo ni jambo muhimu kwa ajili ya utunzaji wa mazingira ili kujikinga na maradhi mbalimbali yanayoweza kuzuilika. Wakati juzi siku hiyo ikiadhimishwa, inakadiriwa kuwa takriban watu bilioni 3.5 duniani wanaishi bila vyoo salama.

Kutokana na takwimu hizo, ni dhahiri kwamba nchi za Afrika ni miongoni mwa nchi zenye watu wanaoangukia katika kundi hilo, hivyo ni muhimu kuongeza kasi kuhakikisha matumizi sahihi ya vyoo bora yanahimizwa ili kuokoa jamii katika kukumbwa na maradhi ya mlipuko.

Katika kutambua umuhimu wa vyoo, miaka ya karibuni kumekuwa na kampeni mbalimbali ikiwamo ya 'Nyumba ni Choo' ambayo ilikuwa ikihamasisha kila kaya kuwa na choo bora. Kampeni hiyo ilienea mijini na vijijini na kufanikisha ujenzi wa vyoo vya kisasa na hatimaye kupunguza maradhi na vifo vitokanavyo na matumizi yasiyo sahihi ya vyoo hasa magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu, homa za matumbo, kuhara na kuhara damu.

Katika kampeni hiyo pia kulikuwa na amri kwamba mtu atakayekutwa akijisaidia ovyo ama njiani au vichakani, akamatwe na kutozwa faini au kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Wakati juzi Siku ya Choo Duniani ikiadhimishwa, nchini Tanzania ilielezwa kuwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii wamekuwa na mchango mkubwa wa utoaji wa elimu ya afya kuhusu umuhimu wa matumizi ya vyoo katika kuepuka na magonjwa ya mlipuko yanayosababisha kujisaidia ovyo vichakani.

Wahudumu hao wamekuwa wakitoa elimu ya afya katika ngazi ya jamii kuhusu matumizi ya vyoo wakishirikiana na maofisa afya, ikiwamo umuhimu wa kunawa mikono baada ya kutoka kujisaidia ili kuepukana na maradhi kama homa ya matumbo na kipindupindu. Elimu hiyo wanayoitoa imesaidia kwa kiasi kikubwa jamii kuwa na uelewa mpana kuhusu matumizi ya vyoo na kuimarisha afya zao. Kwa elimu hiyo, idadi ya wagonjwa na vifo vitokanavyo na magonjwa ya mlipuko vimepungua kwa kiwango kikubwa.


Katika kuonesha kuwa elimu hiyo imewafikia wengi na kuongeza uelewa, shuhuda zilitolewa na baadhi ya wananchi katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma kwamba ina umuhimu mkubwa kwa kila mmoja hasa kwa kuzingatia matumizi sahihi ya vyoo. Wananchi hao walisema kujisaidia vichakani kuna athari kubwa kwa binadamu ikiwamo kung'atwa na nyoka na wanyama wakali pamoja na athari ya kueneza magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu.

Kuna msemo miongoni mwa jamii kwamba kupika chakula ni jambo moja lakini ili kiive mpishi anapaswa kuchochea mara kwa mara. Kwa mantiki hiyo, pamoja na elimu na uelewa wa wananchi kuhusu matumizi sahihi ya vyoo, elimu zaidi haina budi kuendelea kutolewa.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba katika baadhi ya maeneo, mijini na vijijini, bado kumekuwa na changamoto ya magonjwa ya mlipuko hasa nyakati za mvua jambo ambalo limekuwa likichangia matatizo ya afya na hata vifo. Kwa hiyo kasi ya elimu kuhusu matumizi ya vyoo inatakiwa kuongezwa ili kufanikisha lengo la usafi wa mazingira endelevu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Yasmine Protace

## Muungwana Lazima Nilonge

# Msimu juisi, matunda sawa kiafya, ila yapo magonjwa ya uchafu

**KATIKA** kanuni za kiafya, matunda tunatajiwa kuwa yamo katika orodha muhimu ya mlo, kwa manufaa yetu kiafya.

Hilo tunakubali tukiwa na walau ufahamu wa kihistoria, kwamba mtazamo mmojawapo ni kwamba tunapokula matunda, basi tujue tunalinda miili yetu.

Tukirejea katika uhalisia wa kinachoendelea kimaisha ni kwamba, sasa inajulikana kwamba ni msimu wa matunda nchini na yanapatikana kila kona.

Kuanzia sokoni na mtaani tunakopatikana, kuna aina ya mauzo kupitia nyenzo za baiskeli, pia magenge mitaani, sokoni ndiko usiseme inapatikana katika namna mbalimbali.

Kama nilivyogusa awali, kwa nafsi yangu nipazungumzie zaidi Dar es Salaam, mahali niliko. Leo ni msimu wa matunda na wahitaji wako wanapatikana kwa wingi, Hapana shaka wajasiriamali nao wanatumia fursa zilivyo, kuwa wakala wa kuisambaza ziwafikie wahitaji kila waliko, kwao nao mbali na kuwa watoa huduma, wako ndani ya riziki ajira.

Baadhi ya watu wameingia kufanya biashara ya kuuza matunda ya kukata matunda ya kuuza yakiwa mazima huku wengine wakifanya biashara ya juisi. Kila mhitaji kwa staili yake anapata chake.

Hiyo yote ni moja ya watu kujiingizia kipato kupitia biashara hiyo. Lakini, tukisimamia 'vigezo na masharti kuzingatiwa' katika mahali hapo pa kujiingzia kipato, katika sura ya pili inatakiwa wafanyabiashara hao kukumbuka wakati wote usalama wa afya kwa watumiaji, iwe juisi au tunda.

Nina eneo lialonigusa kwa upekee, wauza matunda ya kukatwa. Baadhi yako katika maeneo ambayo si rafiki kiafya, kwa ajili ya kufanyiwa biashara za namna hizo.

Baadhi unakuta taka zimejazana, halafu pembeni mtu kaweka matunda yaliyokatwa kama vile tikiti, nanasi na maembe.

Wapo wanaouza matunda yaliyokatwa na wanayahifadhi katika vifungashio na wapo wanaouza matunda yaliyokatwakatwa na kuyaweka mezani pasipo hifadhi yoyote ya kiafya. Hatari ndiyo inapoanzia hapo!

> Nitumie nafasi hii nihoji, kwa wanaosaga juisi sokoni kukoje, kuanzia juisi yenyewe, maji ya kusaga na usalama wake kwa ujumla ukoje?

Kwa kufanya hivyo wanaotumia vifungashio wanakuwa wamewalinda walaji, lakini kwawanaokata tunda na kuliweka wazi mezani lilivyo, ni wazi hawawalindi walaji tarajiwa. Maana uchafu unafika mahali hapo moja kwa moja.

Kwa upande wao wauza juisi, tunaona wapo baadhi ya wafanyabiashara wanaojali afya za wanywaji juisi.

Anagalizo hilo nalitoa, ilhali kwenye masoko ninawaona waliojiajiri wamewekeza mashine za kusaga juisi, mteja akinunua matunda sokoni na anahitaji kusagiwa anapata huduma hizo.

Hiyo ni hata kabla ya kuchukua chake kama muuzaji au mlaji, anaanza safari yake kwenda kuzitembeza juisi kwa wafanyabiashara walengwa.

Nitumie nafasi hii nihoji, kwa wanaosaga juisi sokoni kukoje, kuanzia juisi yenyewe, maji ya kusaga na usalama wake kwa ujumla ukoje?

Maana tunajua juisi maandalizi yake maji ya yanatakiwa yawe safi na salama. Sasa hao walioko sokoni juisi wanazosaga maji yanayotumiwa. kweli yawe na si ya usalama. Nasema hivyo, maana katika umma tunajuana, kuna wasio na mashine za kusaga juisi, hivyo wanalazimika kusagia sokoni na kwenda nyumbani kujichanganyia maji.

Pia, wapo ambao husaga juisi sokoni na kisha wanajiwekea maji na barafu na kuanza kutembeza mitaani na kuuza. Ndio kigezo cha hatari kinapoanza, pale ikiwa kanuni za kufikia usalama kiafya isipozingatiwa.

Kwa mana hiyo, kunatakiwa suala la usafi lizingatiwe, ili kulinda afya za watumiaji wote na ndipo inabeba tafsiri pana ya usalama wa umma.

Pia na wale wanaokata matunda bila ya kuyafunika na kuuza, nao sio kisiwa, kanuni hiyo inawahusu sana wazingatie usalama wa afya za wateja wao kwa ujumla.

## HABARI KITAIFA

# Tanzania kutimiza lengo la watalii milioni tano

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Pindi Chana amesema mpaka kufikia mwaka 2025 serikali ina uhakika wa kutimiza lengo lake la kuongeza idadi ya watalii na kufikia milioni tano huku mapato nayo yakifikia Dola bilioni sita.

Aliyasema hayo jana wakati wa hafla ya kusaini makubaliano baina ya Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT) na Chuo cha Mafunzo cha Italia (ENAIP). Alisema hatua hiyo ya kuongeza watalii na fedha za kigeni itakwenda pamoja na kuimarisha huduma mbalimbali za watalii kama miundombinu na ujenzi wa hoteli za kisasa.

"Leo tunashuhudia mkubaliano kati ya NCT na Italia ambayo yatatusaidia kuongeza ujuzi kwa upande wa utalii wa mapishi ya vyakula vya aina mbalimbali na lugha ya Kitaliano," alisema.

Alisema makubaliano hayo ni muhimu kwa taifa kwa kuwa yatawapa ujuzi muhimu vijana wa Tanzania na alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuongeza mchango wa sekta ya utalii kwenye pato la taifa mpaka kufikia asilimia 16.

Alisema Italia na Tanzania zimekuwa na uhusiano mzuri wa kiuchumi kwa miaka mingi na kusainiwa kwa makubaliano hayo ni ushahidi wa kutosha na unaendelea kuimarika. Mkuu wa chuo cha NCT, Dk Florian Mtey, alisema ushirikiano huo utakinufaisha chuo chake kwenye eneo la mafunzo na wanatarajia wakufunzi wa chuo hicho watakenda kujifunza kwenye vyuo vya Italia.

Alisema wakufunzi watajifunza programu mbalimbali za masuala ya utalii na ukarimu pamoja na kujengewa uwezo kwenye masuala yaa tafiti na namna ya kuandika miradi.

Aidha, alisema wanafunzi wa NCT watakuwa wakienda Italia kusoma kwenye vyuo mbali vya nchi hiyo kujifunza kwa vitendo na tayari wakufunzi wanaosoma mapishi kutoka nchini Italia wameshaanza kuja nchini.

"Kuna wapishi wa Italia ambao tayari wako nchini na wanatoa mafunzo ya mapishi kwa wanafunzi wetu na watatusaidia wanafunzi wetu kubobea kwenye masuala ya mapishi," alisema.

Alisema NCT kwa kushirikiana na ubalozi wa Italia nchini Tanzania wanatarajia kuanzisha mafunzo ya lugha ya Kitaliano chuoni hapo kwa kuwa kuna soko kubwa linalotokana na ongezeko la watalii kutoka nchini Italia.




Waziri wa Maliasili na Utalii, Pindi Chana (wa pili kulia), akimvalisha vazi la Kimasai Mkuu wa Chuo cha Mafunzo Italia (ENAIP), Antonino Zigilo, wakati wa kusaini mkataba wa ushirikiano na Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Serikali kugawa ekari mil. 4.3 kwa wachimbaji

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imechukua eneo la ekari milioni 4.3 lililokuwa likishikiliwa na watu 11 ambao waliliacha muda mrefu bila kuliendeleza na itagawa kwa wachimbaji wadogo wa madini na kuwapanga wakubwa ambao watafanyia kazi leseni zao.

Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, alisema hayo wakati wa mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji wa Madini 2024, unaofanyika kwa siku tatu mkoani Dar es Salaam ulioanza Novemba 19 utakaomalizika leo, ukiwa na kaulimbiu 'Uongezaji wa thamani kwa maendeleo ya kijamii na uchumi'.

Pia, alisema wamefuta leseni 2,648 ambazo zilikuwa zimeshikiliwa muda mrefu bila kufanya kazi na kupotezea nchi mapato na katika kuwasaidia wachimbaji wadogo, Rais Samia Suluhu Hassan alielekeza Shirika la Madini Tanzania kununua mitambo ili kuwasaidia kuchoronga, akieleza kuwa mpaka sasa zimeshanunuliwa tano na kugawanywa kikanda.

"Pia mwezi huu zitaingia mashine zingine 10 na kufanya idadi kufikia 15 ambazo pia zitagawanywa kikanda, lakini Rais Samia ametoa maelekezo mahususi mashine mbili za uchorongaji zipelekwe kwaajili ya kinamama na vijana ili kuona namna ya kuwainua na kuwaendeleza," alisema Mavunde.

Msingi wa maelezo ya ununuliwa mashine hizo ulitokana na kauli ya Makamu wa Rais wa Shirikisho la Chama cha Wachimbaji Wadogo wa Madini Tanzania (FEMATA) Victor Tesha, aliyeomba serikali kuwapatia mashine za uchorongaji za kutosha angalau moja kila wilaya.

Alisema mashine hizo zitasaidia wachimbaji kupata data za kutosha na kujua kwenye eneo lake kuna mwamba mkubwa kiasi gani, huku akiomba leseni zilizofutwa zitengwe mahususi kwaajili ya kupatiwa wachimbaji wadogo ili kuongeza mchango wao katika Pato la Taifa kutoka asilimia 40 hadi 60.

"Pia, tunaomba vyama vya wachimbaji ambavyo viko chini ya shirikisho la FEMATA wapate ruzuku, kwa kuwa tutavisaidia kuwa na nguvu, mtaona tija inaongezeka katika uzalishaji wa dhahabu na mambo mengine yatazidi kuwa mazuri," alisema Tesha.


Wakati huo huo, Waziri Mavunde alieleza kuwa mazingira ya biashara yamezidi kuimarika na awali ilidhaniwa kuwa uwekezaji ungepungua, lakini hadi sasa hakuna mwekezaji aliyeondoka badala yake wanazidi kumiminika nchini.

"Hii ni ishara kwamba zile falsafa za 4R za Rais Samia zinafanya kazi vizuri na zinavutia uwekezaji nchini, pia ukuaji wa sekta ya madini umeongezeka hadi asilimia 11.3 kutoka 9.3 2021. Mchango katika Pato la Taifa 2021 ulikuwa asilimia 7.2 sasa imeongezeka hadi 9.0 kwa mwaka wa fedha 2024/25.

"Pia makusanyo ya maduhuli yameonyezeka mwaka 2015/16 katika mfuko mkuu wa serikali ziliingizwa Sh. bilioni 161, sasa hivi 2024/25 kwa siku 135 za mwaka wa fedha zimeingizwa Sh. bilioni 392, na lengo ni kuingiza Shilingi trilioni moja ifikapo Juni 2025," alisema Mavunde.

## KABWELA

**Na Fadhil Mohammed**



TANGAZO

## THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

## PRESIDENT'S OFFICE
## PUBLIC SERVICE RECRUITMENT SECRETARIAT

**Ref.No.JA.9/259/01/A/93** **8th November, 2024**

# VACANCY ANNOUNCEMENT

**1.0 BACKGROUND INFORMATION**
On behalf of Prime Minister's Office, Public Service Recruitment Secretariat invites dynamic, proactive, experienced and suitable qualified Tanzanians to fill one (1) vacant post of the Executive Director of Tanzania Commission for AIDS (TACAIDS).

**2.0 TANZANIA COMMISSION FOR AIDS (TACAIDS)**
The Tanzania Commission for AIDS (TACAIDS) is established under the Tanzania Commission for AIDS Act No.22 of 2001 as amended by the Tanzania Commission for AIDS (Amendment) Act No. 6 of 2015 herein after called the Act. The main function of TACAIDS is to coordinate the National HIV and AIDS Mult-Sectoral response in Tanzania. It is responsible for coordinating and overseeing all efforts related to HIV prevention, treatment, care, and support across the country. According to the Act, TACAIDS is an Independent Department under the Prime Minister's Office.

| | |
|---|---|
| **POST** | **EXECUTIVE DIRECTOR** |
| **EMPLOYER** | **TANZANIA COMMISSION FOR AIDS** |
| **REPORTS TO** | **PERMANENT SECRETARY OF THE PRIME MINISTER'S OFFICE** |
| **POSITION OVERVIEW** | The Executive Director is responsible for the overall leadership and management of TACAIDS' performance, coordination and administrative functions. Working under the guidance of the Commission, the Executive Director defines the Commission Vision, Mission and its Strategic Plan, and is accountable for its implementation and the results achieved. The Executive Director is appointed by the President after going through a recruitment process and must abide by the terms specified in the letter of appointment. The Executive Director is the Chief Executive and Accounting Officer of the Commission and is responsible for its day-to-day operations, providing strategic leadership, direction, and management oversight to ensure the effective implementation of the organization's mandate. |
| **WORK STATION** | The Office of the Executive Director will be based at its Headquarter in Dodoma, Tanzania. |
| **DUTIES AND RESPONSIBILITIES** | i. To formulate policy guidelines for the response to HIV and AIDS epidemic and management of its operationalization through the National Strategy in Mainland Tanzania;<br>ii. To develop Strategic Framework for planning of all HIV and AIDS control programmes and activities within the overall National Multi-Sectoral strategy;<br>iii. To foster National and International linkages among all stake holders through proper co-ordination of all HIV and AIDS prevention control programmes and activities within the overall national strategy;<br>iv. To mobilize, disburse and monitor resources and ensure equitable distribution;<br>v. To disseminate and share information on HIV and AIDS epidemic and its consequences in Tanzania on the programmes for its prevention and control;<br>vi. To promote research, information sharing and documentation on HIV and AIDS prevention and control;<br>vii. To promote high level advocacy and education on HIV and AIDS;<br>viii. To monitor and evaluate all on-going HIV and AIDS activities;<br>ix. To coordinate all activities related to the management of the HIV and AIDS epidemic in Tanzania as per National Multi-Sectoral Strategy;<br>x. To facilitate efforts to find a cure, promote access to treatment and care, and develop vaccines;<br>xi. To protect human and communal rights of people infected with and affected by HIV and AIDS in collaboration with relevant sector;<br>xii. To promote positive living of people living with HIV and AIDS;<br>xiii. To advise the government on all matters relating to HIV and AIDS prevention and control in Mainland Tanzania;<br>xiv. To identify obstacles to the implementation of HIV and AIDS, prevention and control policies, programmes and ensure the implementation and attainment of programmes, activities and targets;<br>xv. To supervise all activities related to the prevention and control of HIV and AIDS epidemic and in particular regarding to; health care and counselling of HIV and AIDS patients; the welfare of the orphans and other survivors of the people infected with HIV and AIDS; handling of social, economic, cultural and legal issues related to AIDS epidemic;<br>xvi. Build and maintain effective partnerships with government agencies, NGOs, Donors, and other stakeholders to enhance collaboration and coordination in the HIV and AIDS response;<br>xvii. Ensure compliance with relevant Laws, Regulations, and Guidelines governing the operations of TACAIDS;<br>xviii. Manage the organization's Budget, resources, and financial performance to achieve optimal results and accountability;<br>xix. Represent TACAIDS at National and International forums, conferences, and events to raise awareness and advocate for HIV/AIDS-related issues;<br>xx. Prepare and present regular reports to the Commission and Prime Minister's Office on the Commission's performance, achievements, and challenges; and<br>xxi. In collaboration with relevant sectors perform such other activities and functions relating to the prevention and control of HIV and AIDS epidemic in Mainland Tanzania as the Commission may deem necessary. |

# TANGAZO

| | |
|---|---|
| QUALIFICATIONS | Master Degree in Public Health, HIV and AIDS or a related field from recognized institutions. Candidate Medical back ground will be an added advantage. |
| WORK EXPERIENCE | Minimum of ten (10) years of work experience in the HIV and AIDS and at least 10 years in Public Health sector Managerial position. |
| SPECIFIC KNOWLEDGE AND EXPERIENCE | 11/20/202411/20/2024<br>ii. The highest reputation known for his high morality, integrity, impartiality, and competence in matters of public health, HIV and AIDS and good governance;<br>iii. Must have qualities of leadership, resilience, a sense of urgency, and strong interpersonal and commitment to confronting HIV/AIDS issues;<br>iv. Excellent writing and communication skills in both English and Kiswahili;<br>v. Capacity to handle emotionally difficult and challenging situations with tact and diplomacy; and<br>vi. Ability to work effectively as a team member, as well as alone. |
| PERSONAL ATTRIBUTES | i. Strong inter-personal skills;<br>ii. Role model of ethical standards and integrity; and<br>iii. Familiarity and ease with a variety of cultures and comfort with diverse groups. |
| REQUIRED COMPETENCIES | **Operational Management Skills: -**<br>i. Exceptional management skills of people, finances and systems, with a proven capacity to motivate and lead a multi-disciplinary management team with.<br>ii. An ability to make sound decisions when required on organizational development, balanced by experience in constructive engagement with staff on change management processes and their value to the organization as a whole.<br>iii. A facilitative approach that enables effective delivery with and through partner organizations.<br>iv. A strong analytical mind and an ability to grasp the nature and direction of the Commission.<br>v. Demonstrated leadership and management skills, with a track record of effectively leading and motivating teams to achieve results.<br>vi. Excellent communication, negotiation, and interpersonal skills, with the ability to engage and influence diverse stakeholders.<br>vii. Proven experience in strategic planning, program management, and resource mobilization; and<br>viii. Knowledge of financial management, budgeting, and monitoring and evaluation processes.<br>**Advocacy and Representation Skills: -**<br>i. Public-speaking and influencing skills.<br>ii. Presence, gravitas, humility and empathy in dealings with partners from a variety of backgrounds; and<br>iii. Understanding of and an ability to strategically lead on resource mobilization activities. |
| AGE LIMIT | Not more 45 years except for those who are in Public Service. |
| TERMS OF EMPLOYMENT | Five (5) Years Contract Renewable Upon Satisfactory Performance and within retirement age of a public servant. |
| REMUNERATION/SALARY SCALE | The Salaries, benefits and remuneration of the Executive Directors shall be paid in accordance with the government scales and public employees standards. |
| APPLICATION TIME LINE | Twenty one days (21) days from the date of the advertisement. |

**3.0 GENERAL CONDITIONS**

i. All applicants must be Tanzanian citizen.
ii. Applicants must attach an up-to-date Curriculum Vitae (CV) having reliable contacts; postal address/post code, e-mail and telephone numbers.
iii. People with disabilities are highly encouraged to apply and should indicate clearly in the portal for Public Service Recruitment Secretariat attention;
iv. Applicants should apply on the strength of the information given in this advertisement.
v. Applicants must attach their certified copies of the following certificates: -
  - Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificates;
  - Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma transcripts;
  - Form IV and Form VI National Examination Certificates;
  - Professional Registration and Training Certificates from respective Registration or Regulatory Bodies, (where applicable); and
  - Birth certificate.

vi. Attaching copies of the following certificates is strictly not accepted: -
  - Form IV and Form VI results slips; and
  - Testimonials and Partial transcripts.

vii. An applicant must upload a recent Passport Size Photo in the Recruitment Portal.
viii. An applicant employed in the Public Service should route his application letter through his respective employer.
ix. An applicant who is retired from the Public Service for whatever reason should not apply.
x. An applicant should indicate three reputable referees with their reliable contacts.
xi. Certificates from foreign examination bodies for Ordinary or Advanced level education should be verified by The National Examination Council of Tanzania (NECTA).
xii. Professional certificates from foreign Universities and other training institutions should be verified by The Tanzania Commission for Universities (TCU) and National Council for Technical Education (NACTE).
xiii. A signed application letter should be written either in Swahili or English and Addressed to Secretary, Presidents Office, Public Service Recruitment Secretariat,
P.O. Box 2320, Utumishi Building-University of Dodoma and Dr. Asha Rose Migiro Buildings - Dodoma.
xiv. Deadline for application is 28th November, 2024;
xv. Only shortlisted candidates will be informed the date of interview; and
xvi. Presentation of forged certificates and other information will necessitate legal action;

**NOTE:** All applications must be sent through Recruitment Portal by using the following address; **http://portal.ajira.go.tz/** and not otherwise (This address also can be found at PSRS Website, Click 'Recruitment Portal')
Released by:

**SECRETARY**
**PUBLIC SERVICE RECRUITMENT SECRETARIAT**



# Maofisa ugani waagizwa kuelimisha kilimo mseto

**Na Rose Jacob,** MUSOMA

MAOFISA ugani mkoani Mara wameagizwa kutoa elimu ya kilimo mseto kwa wakulima ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula, biashara na kipato.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mara, Evans Mtambi wakati akifunga Maonesho ya Tisa ya Kilimo Mseto katika Kituo cha Mafunzo ya Kilimo Mseto kilichopo Kata ya Bweri Manispaa ya Musoma.

Mtambi alisema endapo maofisa hao watatoa mafunzo hayo kikamilifu, pia yatawasaidia wakulima katika maeneo yao kukabiliana na mabadiliko hayo ya tabianchi yanayoendelea kutokea duniani.

Alisema mafunzo hayo yatawasaidia wakulima kuachana na kilimo cha mazo na kutumia eneo dogo kuzalisha mazao mengi, mavuno na kutunza mazingira.

**Zaidi ya watu 3,600 kutoka serikali kuu, watumishi ngazi ya mkoa, wilaya, vyuo, taasisi za fedha na wakulima wameshiriki maonesho hayo.**

"Ili kufanikisha jambo hili maofisa kilimo mnapaswa kuwajibika kutoa elimu kwa wakulima, wahimizeni kupanda miti na kutunza uoto wa asili ili tukabiliane na tatizo hili la mabadiliko ya tabianchi," alisisitiza.

Alisema endapo maofisa hao watawaelekeza wakulima kuachana na kilimo cha mazoea kwa kujikita zaidi kwenye kilimo cha mseto, watapata tija kwa kuzalisha chakula cha kutosha na kuongeza kipato.

Mratibu wa maonesho hayo kutoka Shirika la Vi-Agroforestry, Khalid Ngasa, alisema lengo ni kueneza ujumbe kuhusu mchango wa kilimo mseto kuboresha matumizi bora ya ardhi, kipato cha mkulima na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Alisema zaidi ya watu 3,600 kutoka serikali kuu, watumishi ngazi ya mkoa, wilaya, vyuo, taasisi za fedha na wakulima wameshiriki maonesho hayo.

"Maonesho haya yameenda sambamba na uzinduzi wa mpango mkakati wa shirika wa kipindi cha miaka minne kuanzia 2023/27 na usambazaji wa mpango wa pili wa mkakati wa kilimo mseto nchini 2024/30 uliozinduliwa na Makamu wa Rais, Dk. Philipo Mpango katika Maadhimisho ya Siku ya Misitu Duniani Machi 21, 2024, " alisema Ngasa.

Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Dk. Vincent Naano, alisema wafugaji wamekuwa wakichoma moto mbolea za mifugo yao badala ya kuweka katika mashamba yao kurutubisha ardhi na kupata mavuno duni.



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu) ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi (katikati), akigawa moja ya spika 17 kwa Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Shinyanga Mjini, Anorld Makombe (wa pili kulia) juzi, kwa ajili ya wagombea wa CCM kuzitumia katika kampeni za uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji, unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Waandishi watakiwa kudumisha amani

**Bila hivyo, utakuwa mwanzo wa mvurugano na kusambaratika kwa familia kuwa na watoto wasio na makazi.**

**Na Elizabeth Faustine,**

MWANZA

WAANDISHI wa habari mkoani hapa wametakiwa kutumia kalamu zao kulinda na kudumisha amani nchini.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Katibu Tawala wa Wilaya ya Nyamagana, Thomas James wakati akifunga kongamano la kudumisha amani kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu na mkuu mwakani.

James alisema katika kongamano hilo lililoratibiwa na Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Mwanza (MPC) kuwa amani ya nchi inaanzia kwa mtu binafsi kasha kwa familia.

Alisema ili familia iwe na amani ni lazima kila mmoja awe tayari kuyajua na kubeba majukumu yake.

Alisema bila hivyo, utakuwa mwanzo wa mvurugano na kusambaratika kwa familia kuwa na watoto wasio na makazi.

Mwenyekiti wa MPC, Edwin Soko, alisema wajibu wa vyombo vya habari kusimamia misingi ya taaluma na kuwa na uhuru usio na mipaka bila kuathiri haki ya mtu mwingine.

Kiongozi wa Huduma ya Matengenezo Ulimwenguni, Augustine Tengwa, aliwasihi waandishi wa habari kuwa wazalendo kwa kuandika habari na makala katika vyombo vyao vya habari kuhimiza amani ya Taifa ili wananchi wafarijike mioyo na kuendelee kuilinda.

Mmoja wa washiriki wa kongamano hilo, Hellen Daudi, alisema jukumu la kulinda amani ya Taifa ni la kila mwananchi na kuahidi kutoa taarifa za dalili za uvunjifu wa amani.

# Mfumo dume kikwazo wanawake kugombea

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MFUMO katika baadhi ya maeneo ya vijijini umetajwa kuendelea kuwa kikwazo kwa wanawake kushiriki kugombea nafasi za uongozi kutokana na imani potofu dhidi yao.

Hayo yalibainishwa na Mwenyekiti wa Kituo cha Taarifa na Maarifa kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) Kata ya Kiloleli, Kwangu Madaha wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ushiriki wa kundi hilo katika uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika nchini Novemba 27, mwaka huu.

Kwangu, alisema alijitokeza kugombea uenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Kiloleli katika uchaguzi huo na kushindwa ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutokana na kile alichodai ni changamoto ya mfumo dume.

"Tatizo la mfumo dume ndani ya jamii bado lipo japo siyo kubwa kama zamani, wakati wa kupiga kampeni kuwania nafasi hiyo wanaume walikuwa wakifanya kampeni za kunichafua na kueneza maneno kijiji hakiwezi kuongozwa na mwanamke," alidai.

Alidai changamoto nyingine iliyokwamisha kushinda nafasi hiyo kuwa ni kukosa fedha za kuhonga wajumbe kununua kura.

Alisema licha ya tatizo hilo, jamii imeanza kuwaelewa kwani katika uchaguzi huo, alishika nafasi ya pili na kuwabwaga wanaume kati ya tisa.

Neema Shija, alisema wakati akigombea ujumbe wa serikali ya kijiji hicho ndani ya CCM, aliahidi kuitumikia jamii na kusukuma ajenda za wanawake na watoto ndani ya vikao vya maamuzi.

Jenifa Joseph kutoka Kituo cha Taarifa na Maarifa TGNP Kata ya Kiloleli, alisema alikuwa mhamasishaji juu ya wanawake kujitokeza kuwania uongozi kwenye uchaguzi wa huo na kupata muitikio mkubwa na kwamba wanawake sita wameshinda katika kura za maoni, moja nafasi ya uenyekiti.

Joseph Solea, alisema jamii bado inahitaji kupewa elimu dhidi ya mfumo dume na kuwapa nafasi za uongozi wanawake kwa kuwa ni watendaji kazi wazuri na waaminifu.

**Tatizo la mfumo dume ndani ya jamii bado lipo japo siyo kubwa kama zamani, wakati wa kupiga kampeni kuwania nafasi hiyo wanaume walikuwa wakifanya kampeni za kunichafua na kueneza maneno kijiji hakiwezi kuongozwa na mwanamke.**

ama
ALHAMISI NOVEMBA 21, 2024
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**BAKU; KUNAKOFANYIKA COP 29... Mji wa aina yake uliojengwa juu ya meli zilizozama enzi hizo**



**Kijue kisiwa kinachotawaliwa na nyoka na buibui wamejaa kila kona**

Ukurasa 13

## MATAIFA 21 YALIPOKUTANA DAR...

# Dk. Mpango: Awamu Sita imepata umeme Megawati 995 jotoardhi

## •Malengo ya 2030 Mg 5000, vyanzo 52, mikoa 16

**Na Beatrice Moses**

HADI sasa mpango wa serikali nchini ifikapo mwaka 2030 ni kuwa na umeme wa zaidi ya megawati 5,000 kutoka vyanzo tofauti, ikiwamo kutoka kwenye nishati jadidifu za jotoardhi, jua na upepo.

Hayo ni miongoni mwa mambo kadhaa yaliyoelezwa mjini Dar es Salaam mwishoni mwa mwezi uliopita, kwenye Kongamano la Jotoardhi Afrika (ARGeo-C10) lililokusanya washiriki 800 kutoka nchi 21 duniani.

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango katika ufunguzi wa kongamano hilo, akaeleza kwamba ili kufanikisha hayo, serikali inatoa mwaliko kwa wawekezaji kutoka nchi mbalimbali, kuja nchini kuwekeza kwenye sekta ya Nishati ya Jotoardhi, inayozalisha umeme.

Dk. Mpango, pia akataja kuwa itasaidia kuondoa matumizi ya nishati chafu, akifafanua hitaji lililoko ni nguvu ya ziada kutoka kwa wawekezaji, ili kufanikisha upatikanaji wa rasilimali hiyo muhimu kitaifa.

Raia ya Mkuu huyo wa Nchi Msaidizi ni kwamba serikali isiachiwe pekee jukumu, kwani inaiachia ama kizuizi au ucheleweshaji kupatikana nishati hiyo kwa ajili ya lengo lililokusudiwa.

Kwa mujibu wa Dk. Mpango, serikali imeweka mazingira bora, ikiwamo sera nzuri, sambamba na kuwapo uchumi unaokua kwa asilimia tano, hata baada ya kikwazo cha ugonjwa wa Covid 19.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akikagua bidhaa za kimazingira katika kikao cha kimataifa kuhusu joto ardhi, ukumbi wa Mwalimu Nyerere, Dar es Salaam, kikihusisha wajumbe zaidi ya 800. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Anataja kuwapo wataalamu wabobezi katika masuala ya nishati hiyo nchini, hata akatumia nafasi hiyo ya mkutano kuwakaribisha wawekezaji kuendeleza nishati ya jotoardhi katika vyanzo mbalimbali.

**VYANZO VINAVYOTATHMINIWA**

Dk. Mpango anataja vyanzo hivyo vya majini ni mkoani Mbeya kuna Ngozi (Megawati 70) na Kiejo-Mbaka (Megawati 60); Mto Songwe mkoani Songwe, kunakadiriwa megawati tano hadi 35; Mto Natron, mkoani Arusha (megawati 60; na Ruhoi mkoani Pwani, megawati tano.

Pia, anataja Tanzania imeshakamilisha utafiti wa awali kwenye baadhi ya maeneo matano yenye viashiria vya jotoardhi kwenye Bonde la Ufa na sasa kuna uchorongaji unaoendelea katika eneo la Ngozi, ili kuhakiki uwapo wa nishati hiyo.

Makamu wa Rais, anasema serikali inafanya juhudi kuendeleza nishati ya jotoardhi, kwa kuchukua hatua mbalimbali, ikiwamo kuanzisha taasisi maalum ya kusimamia sekta husika, inayopewa jukumu la kusimamia uendelezaji nishati hiyo.

Dk. Mpango anatoa wito kwa viongozi wa Afrika, kuunganisha nguvu zao kushirikiana kufanikisha upatikanaji na matumizi yenye manufaa ya nishati jotoardhi, ambayo ni rafiki kwa mazingira.

Mtazamo wake wa baadaye mkuu huyo ambaye pia ni mchumi kitaaluma, ni kwamba hazina ya jotoardhi inapotumika vyema, itasadia kuacha matumizi ya nishati zisizo safi katika uzalishaji umeme, ikiwamo mafuta mazito.

Anatoa ushauri kwa kila nchi kuwa na taasisi maalum inayobuniwa kitaifa, kwa ajili ya kusimamia uendelezaji wa jotoardhi, pia kuwa na kanuni na sheria zitakazowezesha sekta binafsi kushiriki katika uendelezaji nishati hiyo.

**NENO LA WADAU**

Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais, George Mkuchika, akaeleza katika mkutano huo kuwa sekta ya nishati inaendelea kupiga hatua chini ya usimamizi mzuri wa serikali na hadi sasa umeme nchini umefika vijijini kwa takriban asilimia 98.

Huku umeme vijijini ukihudumiwa na wakala maalum iitwayo REA, Waziri Mkuchika anataja matarajio yaliyopo ni kwamba ifikapo Desemba ijayo, vijiji vyote nchini vitakuwa vimeunganishwa na huduma hiyo ya umeme.

Mkuchika anasema, hatua ya uendelezaji vyanzo mchanganyiko vya nishati ikiwamo jotoardhi inaongezeka, hali ambayo ikisimamiwa ipasavyo, itasaidia kufikisha malengo yaliyowekwa.

Waziri wa Nishati na Mafuta nchini Kenya, James Wandayi, anahimiza uhamasishaji matumizi ya uzalishaji umeme kupitia jotoardhi barani Afrika, kwa kuwa iko endelevu.

Anataja kwamba zaidi ya asilimia 45 ya umeme nchini humo unazalishwa na jotoardhi, hivyo tayari wanaona mafanikio ya nishati hiyo.

Awali, Naibu Waziri wa Nishati nchini, Judith Kapinga, akasema jotoardhi nchini ina nafasi ya kuwezesha azma ya serikali kuwa na umeme unaotokana na vyanzo mchanganyiko.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri huyo, wamekusudia kutimiza lengo la kuzalisha megawati 995 kwa nishati hiyo, ifikapo mwishoni mwaka 2024.

Anaisifu nishati ya jotoardhi ni suluhisho muhimu katika kutatua changamoto za upatikanaji wa nishati ya kutosha barani Afrika, inayoenda sambamba na mipango ya dunia kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa.

Naibu Waziri anasema, jotoardhi ina uwezo mkubwa na inabaki kuwa rasilimali maalum kutoka eneo husika, ikitumika na kuunganishwa katika gridi za kitaifa.

**Inaendelea Uk. 13**

MAZINGIRA

## BAKU; KUNAKOFANYIKA COP 29...

# Mji aina yake uliojengwa juu ya meli zilizozama enzi hizo

## •Mahali panapochimbwa mafuta miaka 70

**Na Mwandishi Wetu**

Ni miongo saba na nusu imepita sasa, eneo katikati ya Bahari ya Caspian kuna kisiwa kilichojengwa kwa nguvu na mkono wa mwanadamu, juu ya Bahari.

Nyenzo zake ni nguzo za minara ya chuma ya kustaajabisha, mabomba, madaraja ya mbao, majengo ya kutoka enzi ya Jamhuri ya Kisoviet (USSR), ambazo hazionekani kwenye ramani.

Historia yake ilianza miaka ya 1940, wakati mtawala Joseph Stalin, aliamuru kufanyike ujenzi, baada ya kugundua kulikuwapo mafuta chini ya bahari ya Caspian.

Ni mahali umbali wa kilomita 55 kutoka eneo la Baku, mwambao uitwao Azerbaijan, ikiwa na maana Kirusi 'Miamba ya Mafuta' pakiweka rekodi kuwa mji wa zamani zaidi katika ukanda wa pwani hiyo kunakozalisha mafuta na umejengwa kwa teknolojia aina yake.

Hapo ndipo kuna mji Baku, penye Kongamano la sasa 29 la Umoja wa Mataifa la Mabadiliko ya Tabianchi mwaka 2024, COP 29, likifanyika na kutarajiwa kumalizika wiki ijayo



Sehemu ya mji wa Baku ulioko juu ya bahari, nchini Azerbaijan. **PICHA: MTANDAO.**

**UJENZI ULIVYOKUWA**

Ulikuwa 1920 Jeshi la kisovieti liliingia Azerbaijan na kuufanya sehemu ya USSR (Muungano wa Soviet) na ikadumu kuwa nayo hadi Oktoba 1991, muda mfupi kabla ya kuvunjika kwa muungano huo.

Wakati wa Vita vya Pili vya Dunia, ilikuwa muhimu kwa mkakati wa kupata nishati kwa USSR, kwani mafuta mengi yaliyotumiwa na kambi ya Mashariki yalitoka Baku.

Awali eneo Neft Dashlari, iliandaliwa kuwa sehemu ya mradi wa miaka mitano uliosimamiwa na mtawala Joseph Stalin, ukiwa sehemu ya miradi ya maendeleo ya uchumi wa USSR wakati huo.

Ilikuwa alama ya usimamizi wa Kisoviet, ingawa mingi haikukamilishwa kutokana na ama kuachwa au kushindikana.

Ujenzi wake ulianza baada ya uchunguzi wa kwanza wa mafuta uliofanikiwa Novemba 7, 1949. Eneo liligeuzwa kuwa moja ya hifadhi kubwa zaidi ya mafuta katika Asia ya Kati na kisima hicho kilitoa mafuta mengi (tani 100 kwa siku), kuashiria uzalishaji wa kwanza

Azerbaijan inabaki kihistoria, ndiyo ya kwanza kuchimba mafuta katika sehemu ya wazi ya Bahari ya Caspian, kwa mujibu wa tovuti ya Socar, mmiliki wa kampuni ya mafuta ya serikali ya nchi hiyo.

Kile ambacho awali kilikuwa eneo ndogo la uchimbaji na nyumba ndogo ya wafanyakazi kukaa huko, kilibadilika kuwa ujenzi mkubwa kuanzia mwaka 1951, ukiitwa "muujiza wa usanifu na kiufundi."

**MSINGI MELI MBOVU**

Ili kuharakisha ujenzi eneo hilo la pwani, kuna ufundi wa ziada ulifanyika kupitia meli zilizokataliwa, zilizamishwa na kutumika kuwa msingi, juu yake nguzo za majengo zilisimikwa.

Mojawapo ya meli hizo ilikuwa aina yake ya mafuta ya kwanza kuwahi kutengenezwa duniani.

Muundaji wake, Ludvig Nobel - kaka wa Albert Nobel, ametengeneza kama suluhisho la kusafirisha mafuta mwishoni mwa Karne ya 19.

"Mnamo 1951 ili kulinda kisiwa hicho kutokana na upepo na mawimbi, meli sita za ziada za kampuni za Khazartanker na Khazardonanma zilibomolewa na kuletwa hapa, zikiwa zimezama nusu na ghuba ya bandia iliundwa kuzunguka kisiwa hicho.

Vyumba vya kuhifadhi meli vilifanywa ukumbi wa mlo, kituo cha matibabu, sehemu ya malazi na matumizi mengine kwa wafanyikazi wachimba visima.

Kwa mujibu wa tovuti ya Socar, hapo ndipo asili ya mji huo kupewa jina 'Kisiwa cha Meli Saba.'Baadaye kisiwa hicho cha bandia kilijulikana kwa jina lake la sasa.

"Mnamo 1951 ili kulinda kisiwa hicho kutokana na upepo na mawimbi, meli sita za ziada za kampuni za Khazartanker na Khazardonanma zilibomolewa na kuletwa hapa, zikiwa zimezama nusu na ghuba ya bandia iliundwa kuzunguka kisiwa hicho.

Kwa miaka mingi, eneo Neft Dashlari, ilipanuliwa kuwa jiji kubwa mfano wa umbo la pweza juu ya bahari, kukiwapo vitalu vya ujenzi kwa wafanyikazi, duka la mikate, maduka, vituo vya matibabu, uwanja wa mpira wa miguu, helikopta na hata ukumbi wa michezo.

Ni kwa mujibu wa Mirvari Gahramanli, Mkurugenzi wa Shirika la Kulinda Haki za Wafanyakazi wa Mafuta linalosimamia haki za binadamu katika sekta ya mafuta na gesi ya Azerbaijan.

**MJI ULIVYO**

Mji huo unatajwa kujengwa mita kadhaa juu ya uso wa bahari na nguzo za chuma zilizowekwa chini ya bahari.

Kunaelezwa kuna majengo ya makazi, idara ya matibabu na usafi na maduka, pia miti imepandwa kwenye vizimba vya chuma na bustani zilizotengenezwa.

Eneo la Oil rocks, lina urefu wa kilomita 12 na upana wa kilomita sita, kulingana na data za asasi ya Gahramanli. Hapo kuna takriban visima 2,000 na wastani wa kilomita 200 za njia zimechimbwa eneo hilo.

Mwanzo kulikuwapo wakati kunaundwa kulikuwapo wafanyakazi wastani 5,000 na sasa kwa mujibu wa Gahramanli, wafanyakazi wako 3,000, ambao mtindo wao wa maisha wanatumia siku 15 baharini na siku 15 nyinginezo kwa mwezi wanakuwa nchi kavu.

**TAASISI HUSIKA**

Inatajwa Neft Dashlarim ni kampuni inayomilikiwa na asasi Socar chini ya miliki ya serikali ya Azerbaijan kunakofanyika mkutano wa Cop 29, ikijishughulisha na uzalishaji, usindikaji na usafirishaji mafuta na gesi, pia inauza bidhaa za mafuta, gesi.

Inaelezwa, kisiwa hicho kilikuwa na manufaa makubwa katika uzalishaji mafuta, ikitoa wastani wa tani milioni 180 za mafuta katika miaka 75 ya kuwapo kwake.

Katika kilele chake mwaka 1967, ilivuka rekodi ya tani milioni 7.6, sasa ikiwa katika tani 3,000 kulingana na takwimu zilizotolewa mnamo Januari mwaka huu.

Kihistoria, kisiwa hicho kilifanikiwa sana katika uzlaishaji mafuta miaka ya 1960, lakini kuanzia muongo uliofuata, miaka 1970 hali ikadilika.

Inatajwa sababu ni kubadilika bei ya mafuta na kuanza kuporomoka thamani ya fedha Dola ya Kisovieti, thamani yake ilianza kupungua.

Pamoja na mageuzi makubwa katika miaka mingi ya kuwapo, alipoulizwa kuhusu hatari ya kisiwa hicho kuzama kutokana na muundo wake au mabadiliko ya hali ya hewa, Mirvari Gahramanli akajibu: "Kisiwa hakiko karibu kuzama na hakuna hatari kama hiyo kwa sasa."

Kimsingi hadi sasa, Neft Dashlari ni kituo cha kimkakati kilichoko baharini, chenye visima na kunafanyika uchimbaji na ujenzi, mitambo.

Inatajwa ikawezekana kufikika kwa helikopta au mashua, ila kwa asili yake, sio mahali panakofika kirahisi au kwa watalii.

Kwa mujibu wa utafiti uliochapishwa, unaelezwa katika ripoti iitwayo 'Communications Earth & Environment', huenda ifikapo mwaka 2100 (miaka 76 ijayo), kisiwa kitaporomoka kwa mita 18, sawa na asilimia 34 eneo la Bahari lililoko.

Katika utafiti huo, wanasayansi walionya maji hayo yatashuka kati ya mita tisa na 18 ifikapo mwisho wa karne iliyopo, hapo kukiendelea utoaji gesi na hewa chafu katika viwango vya sasa.

Hiyo inatokea huku, kikao cha hali ya hewa duiniani kinacjodanaliwa na Umoja wa Mataifa- COP 29, kiko hapo kinajadili mada hiyo, ikiwamo ajenda hali ya hewa ya sasa na baadaye duniani.

Rais mteule wa Azerbaijan, Mukhtar Babayev, anasema kuwa "juhudi za kila mtu" zitahitajika.

• ***Kwa mujibu wa taarifa za kimataifa. Soma zaidi Uk. 14***

MAZINGIRA

# Kijue kisiwa kinachotawaliwa na nyoka, buibui wakazi wake 180

**Na Mwandishi Wetu**



Hoteli ya kisasa katika ufukwe ulioko kisiwani Guam. **PICHA: MTANDAO.**

KISIWA hicho cha Guam kina buibui aina ya guam mara 40 zaidi ya visiwa jirani na idadi kubwa ya nyoka wavamizi na waharibifu mahali hapo, waliojaa katika misitu ambayo ni makazi ya ndege.

Miaka mitano iliyopita, kuliandaliwa mkutano katika kisiwa hicho cha Guam, eneo lenye uchafu mwingi wa kijani kibichi, Magharibi mwa Bahari ya Pacifiki.

Kuna simulizi; ilikuwa jioni, nje kulikuwapo nyama ya nguruwe iliyochomwa, mabaki ya chakula cha jioni. Moto nao ulikuwa unawaka na takriban kila mtu akafika mahali hapo kuzungumza.

Waliporejea, kulikuwapo kiumbe chenye umbo la kahawia lililomzunguka nguruwe, kinang'aa magamba, macho ya wima na mdomo mpana.

Kiumbe huyo alikuwa akipasua vipande vya nyama ya nguruwe na kuvimeza vikiwa vizima, akizimeza polepole.

"Hakuwa nguruwe wa uzito wa kilo 181, lakini alikuwa nguruwe wa kuliwa kwenye karamu kubwa," anasema Haldre Rogers, Profesa Mshiriki katika Idara ya Uhifadhi wa Samaki na Wanyamapori katika chuo cha Virginia nchini Marekani, ambaye amekuwa akitafiti Ikolojia ya Guam kwa miaka 22 iliyopita.

Mgeni huyo 'asiye na adabu' mezani alikuwa nyoka wa kahawia, ambaye anatokana na kuletwa kisiwani Guam katika miaka ya 1940, ikihisiwa ya kupenya kwenye meli ya mizigo.

Kabla ya ujio wake, ndege wengi wa asili walikuwa wakifurahia kuishi katika misitu ya kisiwa hicho, lakini miongo minne tu baada ya nyoka huyo kuingia msituni humo, wawindaji wanaanza kuwamaliza kila mmoja wao msituni.

Kati ya aina 12 waliokuwapo, 10 wameshatoweka kwenye kisiwa hicho, huku aina mbili zilizobaki zikisalia kwenye mapango yasiyofikika na maeneo ya mijini.

Kwa vile sasa jamii ya ndege imeangamizwa kabisa, idadi ya nyoka hao milioni mbili katika eneo hilo la Guam, mlo wao wanategemea panya, mijusi au viumbe kama hao.

''Ninamaanisha watakula chochote''anatamka Henry Pollock, Mkurugenzi Mtendaji wa shirika liitwalo Southern Plains Land Trust, ambaye ana historia ya kuchunguza ikolojia ya Guam.

Guam kukiwa kunapatikana nyoka hao wakali na misitu yenye ukimya mzito sasa, kunasafiri kutoka historia yake ya zamani, sasa kuna sauti na panabaki na kuna umaarufu katika uharibifu wa mazingira.

Hadi sasa inatajwa, madhara ya nyoka wanaoishi mahali hapo, sasa yanaenea zaidi kuwa na misitu ya kutisha isiyo na ndege.

**SIMULIZI BUIBUI**

Buibui wa kisiwani hapo, huku katika visiwa vingine vyenye wasifu kama huo huko Marekani, vyenye ukimya vya Mariana, kuna buibui wachache hasa katika msimu hewa inapokuwa na kavu

Misitu ya kisiwa hicho kina buibui waliotanda karibu kila hatua, wakiwa wakubwa na wenye tumbo la manjano, utando wao wa dhahabu; buibui wenye kutanda, wanaoweka nyuzi za hariri kwenye matundu ya miti.

Rogers anaita aina hiyo mtandao wa "condo", kwa sababu kila moja ni sawa na viumbe wenye miguu minane - wana mamia ya macho yanayometa.

"Huko Guam utando wa buibui, huenda kutoka ngazi ya chini, hadi kwenye dari inaweza kuwa kila mahali," anasema mtaalum Rogers, akiwa na ufafanuzi uanaotajwa kwamba ni mazingira kunapatikana mtandao wa buibui, wengi wa kiume wakizagaa.

Mara nyingi, msitu mzima unaonekana kama umefunikwa na mtando wa buibui bandia kwa ajili ya Halloween.

"Kiasi kwamba unapotembea kwa miguu, ni kawaida kwa mtu aliye mbele kuchukua fimbo ya buibui na kuangusha utando wanapopita," anasema Rogers, akinena "vinginevyo utafunikwa na utando wa buibui ... napenda, lakini ni vigumu kuvuka."

Kila kunapokuwapo uwazi katika miti, eneo lote hilo linajazwa utando kutoka aina tofauti za buibui, wakivutia mwanga kutoka pande tofauti.

Juhudi hizo za pamoja zinatajwa kuweza kuchukua nafasi ya ukubwa wa chumba kwa urahisi. "Nilikuwa na rafiki ambaye alikimbia na kujizungusha tu kwenye utando," anasema Rogers, akifanya hivyo kuwaogopesha aliyokuwa nao.

Hata bila buibui, ambao katika lugha ya asili ya Chamorro hujulikana kama sånye'ye', misitu ya chokaa ya Guam ingekuwa mahali pa kushangaza na hatari, kama pengine popote.

**ARDHI ILIVYO**

Ardhi tajwa, inafafanuliwa kuwa na kuwa na udongo mdogo sana, mimea yake hukua moja kwa moja kwa kulazimisha mizizi yake kwenye mipasuko midogo kwenye miamba na msitu umekaa juu ya mwamba wa kale wa matumbawe.

Pia, Vichwa vya matumbawe bado vinatapakaa kwenye msitu, na mahali ambapo mwamba umemomonyoka, kuna mashimo na mapango.

Nadhani jambo la kipekee ni, kama vile, ni vigumu sana kutembea kwa sababu - hebu fikiria kutembea kwenye miamba iliyochongoka," anasema Rogers.

Anapowapeleka wataalamu wapya kwa ajili ya uchunguzi, wanahitaji muda wa kuzoea eneo hili la mawe - anazungumza kuhusu watu kupata miguu ya baharini - kuweza kutembea bila kuzingatia kila hatua," anasema.

Kwa hivyo, Rogers alipoamua kufanya uchunguzi wa idadi ya buibui mnamo 2012, alijua itakuwa changamoto.

Mara zote kumekuwapo uvumi kwamba, kisiwani Guam kulikuwa makazi ya buibui pekee na hiyo huenda ndio sababu ya kukosekana ndege, ambao kwa kawaida walipenda kula buibui.

Rogers anaeleza kuwa wakazi wa kisiwa hicho chenye takriban wakazi 180,000, hawasafiri hadi Visiwa vingine vya Kaskazini mwa Mariana - wakati kote ni sehemu ya Jumuiya ya Madola; ila Guam ni eneo la Marekani.

• ***Kwa mujibu wa taarifa za kimataifa.***

# DK. MPANGO: AWAMU SITA IMEPATA UMEME MEGAWATI 995 JOTOARDHI

**Inatoka Uk. 11**

Vilevile anataja manufaa yake kwamba, yanaweza kusambazwa kwa usawa kusaidia kukabiliana na tofauti za kijiografia katika upatikanaji nishati, zinazoakisi tofauti kubwa za kiuchumi kitaifa.

Hadi sasa nchini vyanzo vya jotoardhi vinatajwa vipo 52, kwenye mikoa 16, vikitajwa kuwa na uwezo wa kuzalisha umeme usiopungua megawati 5,000.

Kitaalamu inatajwa, katika usambazaji wa nishati ulio sawa, jotoardhi ina jukumu muhimu katika kushughulikia vipimo vya kijiografia vya ukuaji, ikiwaruhusu raia wengi kushiriki na kufaidika na maendeleo ya kitaifa.

Inatajwa kutokana na umuhimu wa rasilimali hiyo, matarajio yaliyoko ni kwamba mkutano huo utaanzisha suluhisho la kushinda vizuizi vinavyozuia maendeleo ya jotoardhi.

Mbunge George Mwenisongole wa Jimbo la Mbozi akiwawakilisha wabunge wanaotoka kwenye mikoa yenye rasilimali ya jotoardhi, anashauri kuwa wananchi wanaoishi kwenye maeneo yenye miradi husika, wapewe kipaumbele cha kuhudumiwa umeme.

Mikoa yenye jotoardhi ni Arusha, Dodoma, Iringa, Morogoro, Mbeya, Kilimanjaro, Kagera, Katavi, Shinyanga, Songwe, Manyara, Rukwa, Singida na Tanga.

Mafunzo yaliyotolewa katika kongamano la ARGeo-C10 kuwa ni pamoja na uendelezaji wa vyanzo vya Jotoardhi na teknolojia mpya, athari za masoko ya rasilimali kaboni na matumizi ya moja kwa moja ya jotoardhi katika sekta mbalimbali, ikiwamo kilimo na ufugaji hasa wa samaki.

MAZINGIRA

## ALICHONADI BAN KIMOON KWA JK...

# Sasa ajenda za COP 29 zinahamia nyumbani kwenye utalii na madini

**Na Peter Orwa**




Viongozi wa kitaifa wanaohudhuria kikao cha hali ya hewa, mjini Baku, Azerbaijan. **PICHA ZOTE; MTANDAO.**

MAMBO yanazidi kuiva katika kikao cha kupigania hali ya hewa iboreke duniani, huko mjini Baku, nchini Azerbaijan, nchi zinazoendelea, ikiwamo Tanzania zinaona mada zinavyozigusa moja kwa moja.

Kwa namna ya pekee, bendera ya kongole inauangukia Umoja wa Mataifa, mwasisi na mwendeshaji wa vikao hivyo. Kwa ujumla wake, si hoja ya jana wala juzi, ina mzizi wake mrefu, Ban Ki Moon, Katibu Mkuu wa zama hizo akiwa na upekee wake kubuni kitu hicho.

Baada ya kuasisi wazo, alipata shida namna atanavyoinadi na kama itakamilika. Akapangia mkakati kutoka nchi moja hadi nyingine, lakini katika sura yake ya kina wanufaika wakuu, nchi zinazoendelea.

Sasa kinachoendelea, daima hakijawahi kuliacha kundi hilo la dunia, ikiwamo kinachoendelea wakati huu tangu kuanza kikao yapata wiki na nusu sasa.

Akiwa ameshapanga ajenda yake ya ushawishi kati ya bara moja na lingine wakati huo, kila moja 'akimwingilia' kulingana na falsafa zake, Ban Ki Moon mnamo katikati ya mwaka 2014, alitua ghafla kisiwani Malabo, mji mkuu wa Guinea ya Ikweta, ambako Waafrika walikusanyika kuteta katika umoja wao, AU.

Ni bahati kamati ya AU inayohusika na hali ya hewa, Mwenyekiti alikuwa swahiba wa karibu wa Ban Ki Moon, Rais Jakaya Kikwete, huku Ofisi ya Makamu wa Rais, anayeshikilia mazingira ni Rais wa sasa, Dk. Samia Suluhu Hassan.

Ban Ki Moon, alipotua akakutana na kamati hiyo ya Kikwete kwa faragha, akifafanua wamekuwa wakiteta kila mara namna ya kuisuka ajenda kuupata Mkataba wa Paris. Hapo akawaibia siri, Waafrika wachangamke kuiunga mkono.

Akawatumia takwimu namna maendeleo ya viwanda na teknolojia zingine zina athari kubwa ya hali ya hewa kwao Waafrika, wakichangia wastani asilimia 15 na iliyobaki nchi zilizoendelea, lakini wao ndio wanaothirika zaidi.

Ban Ki Moon, akifuatana na rais mtaafu wa Ghana katika ajenda hiyo, akawadokeza kwamba 'alishamweka sawa' Rais wa Marekani Barack Obama, kumsaidia kupitisha hilo kwake, naye akiahidi kuwasuka wadau wake wa kisiasa matajiri wamiliki wa viwanda.

"Wabishi ni wale wa Ulaya (EU), lakini nikitoka hapa (jijini Malabo) naenda kukutana nao," akatamka Ban Ki Moon, akiwaomba Waafrika wamuunge mkono kupitisha hoja kwenye kikao cha kwanza kilichotarajiwa kufanyika jijini Washington, Marekani Septemba mwaka huo (miezi mitatu baadaye).

Hapo ndipo Mwenyekiti Rais Kikwete, aliporejeshewa kipaza sauti kunadi ajenda anayojua kwa kina, awagawie Waafrika wenzake, akiwatamkia wana-kikao: "Sasa Waafrika sikilizeni wenyewe... kila siku nikiwaambiaa mnaleta mawaziri wasio na maamuzi, siku zote tunaishia kuwa na Mengistu (Haile Mariam- aliyekuwa Waziri Mkuu Ethiopia) ... Tupigane!".

Ni bahati ajenda ilipita kwa hamasa kubwa kikao cha Washington na hata kikao cha Paris, Ufaransa mwaka uliofuata ikahalalisha rasmi kuwa Mkataba wa Paris.

### KINACHOENDELEA SASA

Sasa ni miaka tisa, utekelezaji wake unasonga kupitia ajenda za vikao vya kila mwaka vinavyoitwa COP, vikiwa na ajenda za maendeleo makubwa kwa nchi zinazoendelea.

Wakati vikao vinaaza huko Baku wiki iliyopita, kulikuwapo misukumo ya wanaharakati kuyataka mataifa makubwa kutoa pesa za kutimiza malengo hayo, huku ndani ya kikao ikiwa moja ya ajenda muhimu.

Katika mambo ambayo sasa ni muhimu yanajadiliwa, ni ajenda inayoiguisa moja kwa moja Tanzania ""madini ya kimkakati namna yanagusa tabianchi na mazingira; na kwanini yanaitwa madini yanaitwa ya kimkakati?"

Wakati mkutano huo wa COP29 ukiendelea huko Baku, Azerbaijan, Mtanzania Adam Anthony, Mkurugenzi Mtendaji wa Haki-Rasilimali, anayehudhuria ana ufafanuzi wake.

Anayataja madini hayo ya kimkakati yamekuwa yakitajwa sana kuwa majawabu makuu katika kuhimili na kukabili madhara ya mabadiliko ya tabianchi.



Mtanzania Adam Anthony, Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya HakiRasilimali, aliyeko Baku, Azerbaijan, katika kikao cha COP29.

Priscilla Lecomte, kutoka Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Uratibu wa Misaada ya kibinadamu, ana maelezo yake naye:

"Mimi niko hapa Baku kwa ajili ya kufuatilia zaidi mazungumzo kuhusu madini ya kimkakati au 'critical minerals' ambayo ni muhimu sana katika kipindi hiki cha 'kuhama kwa nishati', yaani kutoka nishati kisukuku au nishati chafu na kuelekea katika nishati jadidifu au 'renewable energy'..."

Adam anataja madini hayo ya mkakati kwa Afrika, ikwamo nchini Tanzania ni fursa ya kuhama kutoka nishati chafu, pia kutanua wananchi, akidokeza pia yana changamoto zake, akitaja baadhi; kimazingira, kiafya, haki za binadamu.

Anataja kuguswa sana na Ripoti ya Jopo lililoundwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres, iliyozinduliwa Baku, akinena:

"Imeweka misingi ya namna gani madini ya kimkakati yanaweza kupatikana, jinsi ya kutatua changamoto kwenye sekta ya madini hayo. Mathalani kuongeza thamani ya madini hayo husussan barani Afrika.

"Vilevile, mapendekezo ya kuboresha viwanda vya kushughulikia madini hayo kule yanakochimbwa," anaesema Adam akisema matumaini yake ni kwamba mapendekezo hayo yatatekelezwa.

Adam anaeleza kuwa Tanzania ina madini mengi ya kimakati, ikiwamo ya grafiti yanayopatikana Kusini, na nikeli yanayopatikana Kaskazini.

"Madini haya ni sehemu tu kati ya orodha kubwa ya madini ya kimkakati ambayo ni sehemu muhimu sana katika kutengeneza nishati, pia katika mapinduzi ya kidijitali," anasema Adam.

Pia, anafafanua matumizi yake kwa kauli: "Kwa mfano grafaiti na nikeli hutumika katika betri za kuhifadhi nishati kwenye magari ya umeme. Kwenye mapinduzi ya kidijitali ni madini mengine kama kobalti ambayo hutumika kwenye teknolojia ya simu."

Adam anaendelea "kwenye mkutano kama huu ndio utaweza kuangalia nchi za Afrika zenye madini kama haya zinawezaje kuongeza thamani badala ya kusafirisha tu malighafi."

### HALI YA MAKAZI

Huko huko Baku, kukatoka ufafanuzi kwamba katika nchi zinazoendelea na visiwa vidogo na baadhi ya nchi zenye maendeleo kuna kilio cha kuwapo watu bilioni tatu duniani wanaishi katika mazingira yasiyo rafiki kimazingira.

Mambo ya dharura yanayotajwa yanajumuisha, yamo mipango, uwezeshaji fedha, teknolojia na kujijengea uwezo wa kukabili magumu ya aina hiyo.

Hapo kitaalamu kunaelezwa kwamba, mipango inayoendeshwa ihame kutoka 'vipande' na kuhamia katika mfumo mjumuiko unaozalisha mafanikio ya pamoja.

### UTALII VS HALI HEWA

Tayari kuna mpango kazi wa Umoja wa Mataifa kupitia COP29 cha nchini, ikilenga sekta muhimu kama vile utalii kuwa na sera zinazoendana na mikakati ya kudhibiti mifumo ya hali ya hewa.

Katika hoja hiyo iliyotengwa siku maalum ya mjadala, inalenga Sekta ya Utalii, ikiangalia mambo kadhaa ya kufanyika katika malengo yake:

Eneo mojawapo ni kuanza na marejeo ya ajenda ya hoja hiyo iliyowahi kupitishwa huko Glasgow, Scotland inataka kuimarishwa hatua katika kuboresha mifumo ya hali ya hewa kitaifa kwa nchi mbalimbali, mifumo ya kujitolea, utawala wake kuimarishwa, huku wadau wakiwa mstari wa mbele kufanikisha ajenda hizo.

Pili, kunasisitizwa kuimarishwa mifumo ya kisayansi katika kushugulikia hali ya hewa na utalii, ikitengenezwa zaidi miundo ya kitakwimu ya Umoja wa Mataifa inayopima uimara wa utalii, ikiendana na mifumo ya gesi ya kijani.

Pia, kuwapo Taasisi ya Umoja wa Mataifa inayoratibu na kujenga ubia katika namna ya uendeshaji wa taasisi hiyo ndani ya mifumo ya chombo hicho cha kidunia, ili itoe matokeo chanya.



# Uagizaji mbegu kufanyika kidijitali

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) na wadau wa uzalishaji mbegu wameanza mkakati wa kuweka mfumo wa kidijitali kuagiza na kutoa leseni za aina za mbegu nchini.

Wadau hao wakiwemo wataalam kilimo kutoka taasisi za mbegu walikutana jana jijini hapa kujadiliana kuhusu mbinu sahihi za kutekeleza mkakati huo.

Mkutano huo ulioandaliwa na TARI ulipewa jina la "Seed System Digitization, Variety Ordering and Licensing" ha kuhudhuriwa na wataalamu wa mbegu kutoka Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu Tanzania (TOSCI) na Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA).

Wengine ni Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA), Kituo cha Kimataifa cha Uboreshaji wa Mahindi na Ngano (CIMMYT), na Kituo cha Kimataifa cha Kilimo cha Kitropiki (CIAT).

Wengine walioshiriki ni wadau wa mbegu kutoka Uganda na wataalam wa mfumo wa kidijitali wa ubunifu wa mbegu kutoka India na kampuni za ndani ya wazalishaji wa mbegu wa sekta binafsi na maofisa wa Wizara ya Kilimo.

Akizungumza kaika kikao hicho, Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Thomas Bwana, alisema kimeandaliwa kwa ajili ya kuunda jukwaa kutafuta namna bora ya kuweka mfumo wa kitaalamu wa kidijitali kusaidia kusambaza taarifa kwa wadau.

"Lengo ni kupekua maeneo matano muhimu kwa jicho la kuboresha mfumo wa mbegu nchini," alisema Dk. Bwana.

Mgeni rasmi, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao Wizara ya Kilimo, Nyasebwa Chimagu, alisema mpango huo utachukua jukumu kuboresha utendaji wa sekta ya mbegu nchini.

Chimagu, alisema upatikanaji wa mbegu bora kwa wakulima ni hitaji la msingi kuongeza tija katika Sekta ya Kilimo.

# Mameneja mikoa TARURA wapewa angalizo mafuriko

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MTENDAJI Mkuu wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), Victor Seff amewataka mameneja wa mikoa kusimamia ukarabati barabara na kusafisha madaraja ili kunusuru kusombwa na mafuriko msimu wa mvua.

Seff aliyasema hayo katika kikao cha mameneja wa mikoa kilichofanyika katika ofisi za TARURA zilizopo jijini hapa.

Alisema amepita kwenye baadhi ya mikoa na wilaya na kushuhudia baadhi ya barabara hazijafanyiwa ukarabati na madaraja hayajasafishwa.

Alisema kila meneja wa mkoa anapaswa kusimamia eneo lake na mameneja wa wilaya katika maeneo yao ili kutekeleza majukumu yao.

**Nendeni mkafanye kazi yenu kwa weledi ili kulinda taaluma yenu, mkafanye kaguzi za mara kwa mara kwenye madaraja kuhakikisha yanakuwa katika ubora unaotakiwa.**

Seff, alisema mameneja hao, wanapaswa kuzingatia sheria na kanuni ili kufanya kazi yao iwe bora na kulinda sifa ya taaluma yao katika maeneo.

"Nendeni mkafanye kazi yenu kwa weledi ili kulinda taaluma yenu, mkafanye kaguzi za mara kwa mara kwenye madaraja kuhakikisha yanakuwa katika ubora unaotakiwa,"alisema Seff.

Aliwasisitiza kufanya ukaguzi mara kwa mara katika miradi ya barabara na madaraja yanayotumiwa na wananchi ili kuhakikisha yanakuwa imara.

Alisema barabara ni muhimu kwa matumizi ya wananchi kuendesha shughuli zao za kiuchumi kutoka sehemu moja kwenda nyingine, hivyo hazipaswi kuachwa bila kufanyiwa matengenezo.

Mkurugenzi wa Huduma Saidizi wa TARURA, Azimina Mbilinyi, aliwataka mameneja hao kuwasimamia watumishi walio chini yao kwenye utunzaji wa vifaa vya kazi ili vidumu na kutumika kwa muda mrefu.

Vilevile, aliwataka kutunza siri za kazi, kujenga ushirikiano na taasisi nyingine zinazowazunguka kwenye mikoa yao kitendo hiko kitawasaidia kufanya kazi yao vizuri.

Seff, alisema jamii inaitegemea TARURA katika masuala ya barabara, hivyo wakiwa wanafanya kazi zao wanapaswa kukumbuka kuwa kuna wananchi wanategemea barabara ili kuendesha shughuli zao.



Fundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA), Emmanuel Lugembe (kushoto), akitoa maelezo kwa wajumbe wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC), walipotembelea chanzo cha maji Mzakwe, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Uchumi waendelea kuimarika nchini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema uchumi wa nchi umeendelea kuimarika katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Septemba mwaka huu.

Ni baada ya kutoa mwenendo wa viashiria vya kiuchumi vya muda mfupi kwa kipindi hicho katika Sekta ya Utalii, Nishati na Mawasiliano.

Mkurugenzi wa Takwimu za Uchumi Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Daniel Masolwa, akitoa taarifa hiyo kwa waandishi wa habari juzi jijini hapa, alisema mwenendo wa viashiria vya uchumi nchini umeendelea kuimarika.

"Katika kipindi cha Januari hadi Septemba, 2024 taarifa hii inaonyesha mwenendo wa baadhi ya viashiria kama idadi ya watalii walioingia nchini iliongezeka hadi milioni 1.5 ikilinganishwa na watalii milioni 1.2 walioingia katika kipindi kama hicho mwaka 2023 ikiwa ni ongezeko la watalii 260, 640 sawa na asilimia 20.0," alisema

Masolwa, alisema idadi ya watalii walioingia nchini katika kipindi cha Januari hadi Septemba kuanzia mwaka 2021 hadi 2024, imeendelea kuongezeka kutoka 624,396 mwaka 2021 hadi 1,560,641 mwaka 2024 ikiwa ni ongezeko zaidi ya mara mbili na nusu ya ilivyokuwa 2021.

"Kuongezeka kwa idadi hii kunatokana na hatua mbalimbali za kutangaza vivituo vya utalii nje ya nchi ikiwa ni pamoja na filamu ya Royal Tour na Amazing Tanzania zilizotayarishwa na serikali ya awamu ya sita kwa lengo la kuongeza zaidi watalii wanaoitembelea Tanzania," alisema

Alisema idadi kubwa ya watalii waliongia nchini kutoka nje ya Bara la Afrika katika kipindi cha Januari hadi Sepemba 2024 na idadi yao kwenye mabano, Marekani (112,579), Ufaransa (79,079), Ujerumani (76,021), Italia (75,543) na Uingereza (67,180).

"Katika kipindi hicho idadi kubwa ya watalii kutoka Bara la Afrika walitoka Kenya (156,674), Burundi (153,497), Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) (49,963) Zambia (46,599) na Rwanda (45,810)," alisema.

Uzalishaji wa Nishati

Akizungumzia kuhusu uzalishaji wa nishati, Masolwa, alisema umeme katika kipindi cha Januari hadi Septemba, 2024 uliongezeka hadi sasa kilowati bilioni 8.5 ikilinganishwa na saa za kilowati bilioni 7.6 zilizalishwa kipindi kama hicho mwaka 2023, ikiwa ni ongezeko la saa za kilowati milioni 893.2 sawa na asilimia 11.8

Alisema kiasi kikubwa cha umeme kilichozalishwa katika kipindi hicho mwaka 2024 kilitokana na chanzo cha gesi kwa asilimia 51.8, maji 46.9 na mafuta 1.2.

"Uzalishaji wa umeme kwa aina ya chanzo katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2024 ulikuwa maji asilimia 60.4, gesi 38.4 na mafuta 1.2. Mabadiliko haya yametokana na kuendelea kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme kwa kutumia chanzo cha maji," alisema

Vilevile, Masolwa, alisema katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2021, mchanganuo wa uzalishaji umeme kwa aina ya chanzo ulikuwa maji asilimia 35.9, gesi 62.9 na mafuta1.2.

Alifafanua kuwa kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme unaotokana na chanzo cha maji umechangiwa na Bwawa la Julius Nyerere, hivyo kupunguza uzalishaji katika gridi ya taifa kwa chanzo cha gesi asilia.

Kuhusu huduma za mawasiliano, alisema Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa sasa ni nyenzo muhimu katika shughuli za kiuchumi kitaifa na kimataifa.

"Huduma hii imekuwa ni kichocheo kikubwa cha kuongeza tija katika uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma katika mnyororo wa thamani," alisema.

Kwa mujibu wa Masolwa, katika kipindi cha Januari hadi Septemba mwaka huu, huduma ya mawasiliano kupitia muda wa maongezi iliendelea kuongezeka hadi dakika bilioni 115.7 kutoka bilioni 105.9 kipindi kama hicho mwaka 2023 ikiwa ni ongezeko la dakika bilioni 9.7 sawa na asilimia 9.2





# Dk. Mpango kuongoza mamia Siku ya UKIMWI Duniani

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani ambayo kitaifa yatafanyika Desemba Mosi mwaka huu katika viwanja vya Majimaji Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma.

Hayo yalisemwa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed wakati akitoa taarifa ya maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani kwa waandishi wa habari ofisini kwake mjini Songea.

**Kwa mwaka 2024 maadhimisho hayo yameanza Novemba 21 hadi Desemba Mosi 2024 ambayo itakuwa ni kilele cha maadhimisho ya Siku ya UKIMWI kitaifa mkoani Ruvuma.**

Alisema kabla ya siku ya kilele kutatolewa huduma mbalimbali ikiwemo za ushauri pamoja na upimaji wa hiyari wa Virusi Vya Ukimwi, kisukari, shinikizo la damu na uwiano wa uzito, uchangiaji wa damu, chanjo ya homa ya ini pamoja na elimu ya lishe.

Alifafanua kwamba huduma hizo zitatolewa katika viwanja vya majimaji na nje ya viwanja hivyo, kwenye halmashauri zote nane za Mkoa wa Ruvuma katika wiki yote ya maadhimisho.

"Kwa mwaka 2024 maadhimisho hayo yameanza Novemba 21 hadi Desemba Mosi 2024 ambayo itakuwa ni kilele cha maadhimisho ya Siku ya UKIMWI kitaifa mkoani Ruvuma," alisema Kanali Abbas.

Aidha, alibainisha kwamba malengo mahususi ya maadhimisho hayo ni kutoa fursa ya kutathmini hali halisi ya mwelekeo wa kudhibiti Virusi Vya Ukimwi kitaifa na kimataifa pamoja na kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu udhibiti wa maambukizi mapya.



"Malengo mengine ni kuendelea kuhimiza huduma stahiki kwa watu wanaoishi na maambukizi ya VVU na kuwakumbuka wale wote waliopoteza maisha kutokana na UKIMWI," alisema Kanali Abbas.

Alisema kaulimbiu ya maadhimisho hayo ni "Chagua njia sahihi, tokomeza UKIMWI" ambayo inakumbusha kuzingatia njia sahihi za kitaalamu katika kujikinga na maambukizi ya VVU ili kutokomeza janga la ugonjwa huo ifikapo mwaka 2030.



Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Prof. Elifas Bisanda (wa pili kushoto), akizungumza wakati akifungua jukwaa la maprofesa wa chuo hicho, lililokutana Bunju, Dar es Salaam juzi, kujadili masuala mbalimbali ya kiutafiti, ubunifu na huduma kwa jamii. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Vipaza sauti vyatumika kukabili ukatili kijinsia

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, imebuni mbinu ya kutumia vipaza sauti na spika kuhamasisha wananchi kuhusu namna ya kukabiliana na tatizo la ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto kwenye makazi yao.

Vifaa hivyo vinatumika kuhamasisha shughuli mbalimbali za maendeleo kwenye vijiji ili kuongeza uzalishaji mali na kuongeza mapato ya halmashauri hiyo.

Halmashauri hiyo imeanza kutekeleza lengo hilo kwa kugawa vifaa hivyo kwa maofisa maendeleo wa kata tisa za wilaya hiyo ili waanze kuvitumia kwenye maeneo yao.

Vifaa hivyo vilikabidhiwa kwa maofisa hao juzi na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Bosco Mwanginde ambaye aliwataka kwenda kuvitumia kwa malengo yaliyoainishwa badala ya kuvitumia kwenye shughuli zingine.

Alisema kwa ofisa maendeleo wa kata ambaye atavitumia vifaa hivyo kwa kazi ambazo ni tofauti na malengo ya serikali atachukuliwa hatua za kisheria.

Kaimu Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ya Chunya, Esther Kondobole alizitaja kata ambazo zimeanza kugawa vifaa hivyo kuwa ni Chokaa, Mbugani, Chalangwa, Sangambi, Matundasi, Makongolosi, Mkola, Mamba na Lualaje.

Alisema wataendelea kugawa vifaa hivyo kwa awamu mpaka watakapokamilisha kata zote 20 za wilaya hiyo, huku akisisitiza kuwa lengo la serikali ni kuwarahisishia utendaji kazi maofisa maendeleo hao.

Alisema vifaa hivyo pia vitakuwa vinatumika kuhamasisha wananchi kuhusu mikopo ya asilimia 10 za mapato ya ndani ambayo ni kwa ajili ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Baadhi ya maofisa maendeleo wa kata ambao walikabidhiwa vifaa hivyo walisema wananchi kuhusu mikopo utekelezaji wa majukumu yao katika kuwahudumia wananchi.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Kata ya Sangambi, Erick Msola alisema awali walikuwa wanatumia vifaa ambavyo vilikuwa duni na havifikishi sauti umbali mrefu.

Alisema vifaa walivyopatiwa ni vya kisasa na vitawasaidia kuwaelimisha wananchi kuhusu masuala mbalimbali ikiwemo shughuli za maendeleo kwenye maeneo yao.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Kata ya Chokaa, Joyce Ephraimu alisema watavitumia vifaa hivyo kutoa elimu kwenye maeneo mbalimbali ya umma ikiwemo kwenye vituo vya mabasi, sokoni na shule za sekondari na msingi.

Alisema kwenye maeneo ya mikusanyiko ndiko ambako huwa ni rahisi kufikisha elimu kwa watu wengi na kwamba vifaa hivyo vikitumika watafikisha ujumbe kwa watu wengi zaidi.

# Madiwani watoa mbinu uboreshaji mikopo 10%

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MADIWANI katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya wameshauri elimu itolewe kwa kina kuhusu mikopo ya asilimia 10, hatua itakayowezesha halmashauri hiyo kukopesha vikundi sahihi ambavyo vitarejesha mkopo kwa wakati.

Aidha, wametaka viongozi wa vijiji kushirikishwa ipasavyo kwenye utoaji wa elimu hiyo kwa madai kuwa wao ndiyo wanawajua wananchi wao kuanzia tabia zao na shughuli wanazofanya.

Walitoa maoni hayo juzi wakati wa kikao cha robo ya kwanza cha baraza la madiwani wa halmshauri hiyo kilicholenga kupitisha ajenda za kamati mbalimbali za baraza hilo.

Diwani wa Kata ya Igoma, Andrew Mwaipopo alisema maofisa maendeleo ya jamii pekee hawatoshi kutoa elimu juu ya utoaji mikopo hiyo kwa maelezo baadhi yao bado ni wageni katika maeneo yao, vile vile hawawafikii wananchi wengi hivyo wanahitaji usaidizi kutoka kwa viongozi wengine.

"Ofisa maendeleo ya jamii na mtendaji, wao wanatoka nyumbani na kwenda ofisini na kama wanawatembelea wananchi ni mara chache. Naamini wengi wao hawajui mazingira ya watu wao ipasavyo lakini wenyeviti ndiyo wanawajua vizuri ," alisema Mwaipopo.

Diwani wa Shizuvi, Noah Mwashibanda alisema kwa sasa kata yake haina ofisa maendeleo ya jamii na kwamba licha ya kuwa na wajasiriamali wengi kwenye kata hiyo lakini hawajapata elimu ya kutosha kuhusu mikopo hiyo.

Hivyo, aliiomba Ofisa Maendeleo ya Jamii kutembelea kata hiyo ili kuwapa elimu wananchi wake kwani hadi sasa vikundi vingi vimeeleza kukosa vigezo vya kupata mkopo kwa sababu havijasajiliwa kutokana na kukosa elimu.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Ezekia Shitindi alimwagiza Ofisa Maendeleo ya Jamii wa wilaya hiyo kuhakikisha anawasimamia watendaji wake ngazi ya kata na kijiji ili kuhakikisha wanatimiza wajibu wao ipasavyo wa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu mikopo hiyo.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri hiyo, Agnes Elikunda, alisema wataendelea kutoa elimu kwa madiwani na viongozi wengine kupitia vikao mbalimbali ili watumike kuelimisha wananchi wao kuhusu utaratibu wa utoaji mikopo hiyo kuanzia kujisajili hadi kupata.



# Mbaroni tuhuma mauaji ya mtoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi Mkoa wa Kusini Unguja linamshikilia Maulid Hassan Maulid (18) mkazi wa Mwera Pongwe kwa tuhuma za mauaji ya mtoto wa miaka sita, Khadija Dadi Nahoda.

Inadaiwa kuwa kabla ya kutekeleza tukio hilo, Maulid alimwingilia kimwili mtoto huyo na kusababisha kifo chake.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake, Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Daniel Shillah, alisema majira ya saa moja asubuhi ya Novemba 14, mtoto huyo ambaye sasa ni marehemu aliondoka nyumbani kwao na kuelekea shuleni huku mama yake akimsindiki za.

**Kabla ya kufika shule mama huyo alimkabidhi kijana mmoja ambaye ni miongoni mwa familia ili amfikishe shule.**

Alisema kabla ya kufika shule mama huyo alimkabidhi kijana mmoja ambaye ni miongoni mwa familia ili amfikishe shule.

Kamanda Shillah alisema kijana huyo hakumfikisha mtoto huyo shuleni, kwamba alimjumuisha na wanafunzi wezake aliowakuta njiani.

Alisema hadi ilipofika majira ya saa 7:00 mchana mtoto huyo hakurejea nyumbani kama ilivyo kawaida yake jambo ambalo lilimpa wasiwasi mama yake na alipouliza shuleni akajulishwa kuwa mtoto wake hakufika shuleni siku hiyo.

Alisema mama huyo alilazimika kutoa taarifa katika Kituo cha Polisi Dunga Mkoa wa Kusini Unguja.

Kamanda Shillah alisema mwili wa mtoto huyo uliokotwa eneo la Mwera ukiwa katika vichaka kwenye jengo ambalo halijakamilika akiwa amefariki dunia.

“Jeshi la polisi kwa kushirikiana na raia liliendelea na upelelezi na kufanikiwa kumkamata mtuhumiwa ambae alibainika kuwa ndiye aliyemkamata mtoto huyo wakati anaenda shuleni, akamziba mdomo na kumuingiza kwenye boma la nyumba na kumwilingilia kimwili na kumsababishia kifo chake” alisema.

Alisema upelelezi wa shauri hilo utakapokamilika jalada litapelekwa kwa Wakili wa Serikali kwa ajili ya hatua za kisheria.

Aidha, aliwataka wazazi na walezi kuwa karibu na watoto wao na kuhakikisha kuwa wanawapeleka na kuwarudisha shuleni ili kutotoa mwanya kwa wahalifu wa matukio maovu.

## Mtoto wa mwaka mmoja aliyepotea apatikana

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

JESHI la Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja limefanikiwa kuwapata watoto wawili akiwamo mwenye umri wa mwaka mmoja, ambao waliripotiwa kupotea tangu Novemba 15 mwaka huu Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, Richard Mchomvu, alisema Novemba 15 majira ya saa 10:00 alasiri katika Kituo cha Polisi Kijito Upele Wilaya ya Magharibi B” Mkoa wa Mjini Magharibi kulipokelewa taarifa ya kupotea kwa watoto wawili ambao ni Fatma Ali Omar (12) mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Kwarara na Swadrat mwenye umri wa mwaka mmoja na nusu.

Alisema baada ya kupokea taarifa hiyo, Jeshi la Polisi lilianza uchunguzi wa tukio hilo ambapo kwa kushirikiana na taasisi nyingine, vyombo vya habari pamoja na raia wema lilifanikiwa kupata taarifa za watoto hao kuwa walienda mkoani Arusha na baadaye kurejeshwa jijini Dar es salaam.

Alisema juzi watoto hao walipatikana wakitokea Dar es Salam, ambapo baada ya mahojiano ya awali, Fatma alieleza kuwa aliondoka nyumbani kwao kwa lengo la kwenda kutembea sehemu yeyote nje ya Zanzibar.

Kamanda huyo alisema watoto hao wamefanyiwa vipimo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na afya zao zinaendelea vizuri.

“Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wa tukio hilo. Aidha linapongeza vyombo vya habari, taasisi mbalimbali zilizoshiriki katika kufanikisha kupatikana kwa watoto hao pamoja na wananchi waliotoa ushirikiano wa taarifa mbalimbali” alisema Kamanda Mchovu.

Akizungumza na waandishi wa habari mama wa watoto hao ambaye hakutaka kutajwa jina lake, alisema tukio hilo liliwatia hofu na wasiwasi kwa sababu watoto wake hawana kawaida ya kuondoka bila ya ruhusa.

Alisema: “Tunashukuru kwamba watoto wetu wapo salama na wamerejea wakiwa na afya nzuri, tunawashukuru wale wote waliofanikisha kuwapata watoto wetu”.




Kamanda wa Polisi mkoa wa Kusini Unguja, Daniel Shilla akizungumza na waandishi wa habari jana, kuhusu tukio la mtoto wa miaka 16 aliyeuawa baada ya kudaiwa kubakwa katika eneo la Mwera, mkoani humo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Tanzania yaihakikishia Australia usalama uwekezaji wa madini

**Na Gwamaka Alipipi**

TANZANIA imeihakikishia Australia mazingira rafiki ya uwekezaji katika sekta ya madini, licha ya kufanyika kwa mabadiliko ya sera, kanuni na sheria za madini zilizofanywa mwaka 2017.

Naibu Waziri wa Madini, Dk.Steven Kiruswa akizungumza kwenye mjadala uliongazia “Uwekezaji wa Australia kwenye sekta ya madini nchini Tanzania” alisema sera, sheria zilizorekebishwa hazitaathiri uwekezaji katika madini kwa wawekezaji wowote watakaokuja kuwekeza nchini.

Alisema serikali inaendelea na mchakato wa kuweka mazingira wezeshi kupitia miongozo,sera, kanuni na sheria katika eneo la uongezaji thamani wa madini.

“Tumewaondolea hofu katika uwekezaji. Kuna timu ya maridhiano katika sekta ya madini imeundwa ambapo Serikali inapata asilimia 16 na mwekezaji anapata asilimia 84,” alisema Dk. Kiruswa.

Alisema mwekezaji yoyote anayekuja kuwekeza katika sekta ya madini ni lazima ahakikishe umuhimu wa ushirikishwaji wa Watanzania.

Alisema pia ni lazima azingatie nafasi za ajira za wazawa pamoja na kutumia bidhaa zinazozalishwa Tanzania, kupewa kipaumbele, kwamba hadi sasa asilimia 97 ya bidhaa zinazotumika katika sekta ya madini zinazalishwa nchini.

Alisema pia madini yatakayopatikana yaongezewe thamani hapa nchini, sambamba na vifaa vyote vinavyotengenezwa kwa madini vianze kuzalishwa hapa nchini.

Dk. Kiruswa alisema sekta ya madini imekuwa ikichangia kwa kiasi kikubwa katika pato la taifa, kwamba kuanzia mwaka 2018 hadi 2022, sekta hiyo ilikua kutoka asilimia 4.8 hadi asilimia 9.1.

Alisema serikali imelenga kukuza mchango wa sekta hiyo ili kufikia mchango wa asilimia 10 katika pato la taifa ifikapo mwaka 2025.

Naye Naibu Balozi wa Australia nchini, Chris Ellinger alisema kwa muda wa miaka miwili Australia imetumia Sh. trilioni 10 katika kufanya utafiti wa maeneo ya kuwekeza katika madini.

Alisema Australia inaongoza duniani kwa kuwekeza katika sekta ya madini, kwamba imekuwa na kampuni nyingi ambazo zimezagaa nchi mbalimbali.

Alisema mkutano huo uliangazia usalama wa kampuni za Australia kuwekeza katika sekta ya madini, kutokana na Tanzania kufanya marekebisho ya sheria, kanuni na sera.

Uhusiano baina ya Australia na nchi za Afrika umekuwa ukiongezeka kutokana na kampuni ya Australia kuwekeza zaidi ya Dola za Marekani bilioni 60 kwenye miradi ya uchimbaji madini.

Kwa Tanzania kampuni 35 ya Australia zimewekeza kwenye utafiti wa madini, uchimbaji, kuongeza thamani na usimamizi wa maafa ya jiolojia.

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**LUCAS NJILE MITIMINGI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye Index namba **S. 2968/0041/2012** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Shule ya Sekondari Langabilili. Cheti hiki kimepotea katika kijiji cha Mtavira wilayani Ikungi mkoa wa Singida. Yoyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi **PHQ/SIN/IKU/9898/2024**

## KUPOTEA KWA VYETI



**ATHUMANI MUSTAPHA MSHIHIRI,** Anatangaza kupotea kwa Vyeti vya Kidato cha Nne,Shule ya Sekondari Lwandai Tanga chenye Usajili **CS18273929**, Index **No:S0584-0079-2018** na Chuo cha Ardhi morogoro Diploma chenye Usajili **DGM22010**, Index **No:S0584/0079/2018** Kwa yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu nae.

**TAARIFA YA POLISI,**
**PHQ/TAN/KOROGWE/12176/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**AISHA SALUMU ABDALLAH** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye majina **CITY BOYS ELECTRONICS CO. LTD** namba za usajili **MC825CBT** aina ya **TVS STAR.** Chassis No. **MD625AF76J1K15097,** Engine No. **AF7KJ1314678.** Yeyote atakayeyiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi:
**PHQ/DOD/DOD/53391/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JUMANNE JUMA MTANDIRA**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T.894 BCN** yenye chassic namba **J100E013652,** engine namba **HC0825593** aina ya Toyota Cami. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya polisi;
**PHQ/ARU/ARU/44704/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LUKIZA JUSTUS MUTUNGI**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T.948 ARW** aina ya Toyota **HILUX SURF.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya polisi;
**PHQ/DAR/KIN/252880/2024.**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 26177 OF 2024**

**IN THE MATTER OF ESTATE OF THE LATE TUMAINI ALPHONCE MABAGALA OF DODOMA CITY**

**AND**

**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**

**ANAWEDI JOSEPH MABAGALA..................1st PETITIONER**

**FOCUS MAGESA....................................2 ND PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 04 day of 12............................2024
Dated at Dodoma this 20 day of 11 ...............2024.

RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha Mjini Mkoa DODOMA**

**Shauri la Madai Na 456/2024**

**Jina la Mdai STEPHEN MUHILA NYAKAPALA**

**Jina la Mdaiwa LESILEE JOSIA MADEHA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa LESILEE JOSIA MADEHA MATUMBURU**
**Kwa kuwa Mdai/Wadaiwa ameleta/Wameleta madai yake /yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai)**

**MADAI YA TSHS. 700,000/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 26 Mwezi 11 Mwaka 2024 Saa 2:30 asubuhi/Mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikilza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehw 20 Mwezi 11 Mwaka 2024.

.................................................
HAKIMU

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**
**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MIRATHI NA 26643 YA MWAKA 2024**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU PRISCILLA STEPHEN GEORGE**

**NA**

**PRUDENCE BASHAIJA TIMANYWA .........MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa waombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 12 Mwezi Kumi na Mbili, 2024 Saa 4.30 asubuhi. Siku ambayo shauri hili limepangwa kusikilizwa Mbele ya Jaji M. MNYUKWA.
Imesainiwa Dar es Salaam, leo tarehe 19 Mwezi wa Kumi na Moja, 2024

NAIBU MSAJILI

---

**IN THE DISTRICT DELEGETE COURT OF LONGIDO**
**AT LONGIDO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO: 28110 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE GOODLUCK NDEKERO MOLLEL**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**NAMAYANI LUCA MARARY**

**GENERAL CITATION**
**(Made Under Rule 75 of the Probate Rules)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 10 day of December, 2024.
No will of the said deceased is deposited at the court
Dated at LONGIDO this 14th day of NOVEMBER 2024.

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE
LONGIDO DISTRICT COURT

RESIDENT MAGISTRATE.

---

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi***
***Kwa Bei Poa***
***Tupigie: +255 - 0677 020701***

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Adaiwa kumuua bibi kwa nyundo, jiwe

**Na Godfrey Mushi, SIHA**

MTU anayedhaniwa kuwa na tatizo la afya ya akili, Ronald Ulomi (36), mkazi wa kijiji cha Ormelili, wilaya ya Siha, Kilimanjaro, anadaiwa kumuua bibi yake kwa nyundo na jiwe, baada ya kuchukizwa na kitendo cha kufungwa kamba mkononi.

Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Simon Maigwa, alisema jana kuwa mtuhumiwa alifanya tukio hilo Novemba 16, mwaka huu.

"Huyu alikuwa anapelekwa hospitalini na mama yake mzazi aitwaye Rahel Munisi. Sasa wakati wanampeleka akawatoroka na kurudi nyumbani. Mke wake akamfungua kamba.

"Baada ya kumfungua, mtuhumiwa alichukua nyundo na kumpiga bibi Akanashe Mushi (85) kichwani na kudondoka chini. Alipodondoka alichukua tena jiwe na kuendelea kumpiga kichwani hadi kumsababisha mauti. Kijana ni kama kichaa," alisema.

Kwa mujibu wa Maigwa, tayari jeshi hilo linamshikilia mtuhumiwa baada ya kutiwa mbaroni wakati akipelekwa hospitalini na mama yake mzazi.

Diwani wa Ormelili, Noel Mollel, akizungumzia tukio hilo, alisema mtuhumiwa kwa muda mrefu hayuko sawa kiakili na alishapelekwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro (Mawenzi) kupatiwa matibabu.

Mollel alisema kabla ya kutokea tukio hilo, usiku aliwakimbiza hapo nyumbani mama yake na bibi huyo na walikwenda kulala kwa majirani.




Waandamanaji wakiwa na picha ya kiongozi wa upinzani wa Msumbiji, Venancio Mondlane, wakati wa maandamano yaliyofanyika hivi karibuni. **PICHA: AFP**

# TGNP yaonya ukatili wa kijinsia uchaguzi wa Serikali za Mitaa

**Na Grace Mwakalinga**

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TGNP), umetoa tahadhari kuhusu ukatili na udhalilishaji dhidi ya wanawake wakati wa kampeni za uchaguzi wa serikali za mitaa.

Badala yake, umewataka wagombea wa vyama mbalimbali kufanya kampeni zinazozingatia haki na utu wa mwanamke wakati wa kampeni hizo.

Wito huo ulitolewa jana na Mratibu wa Mafunzo wa TGNP, Anna Sangai, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu mambo yanayopaswa kuzingatiwa kipindi hiki cha uchaguzi.

Alisema ni muhimu kampeni zikafanyika kwa amani na utulivu ili kulinda haki za binadamu hususani wanawake ambao wamekuwa wakiathiriwa na lugha za udhalilishaji kwenye kipindi cha uchaguzi.

"Tunaviomba vyama vya siasa kuzingatia utu wa mwanamke katika mikutano yao. Sisi kama watetezi wa haki na usawa wa kijinsia, hatupendi udhalilishaji dhidi ya wanawake majukwaani au katika eneo lolote wakati wa kampeni. Tumejipanga kushiriki kikamilifu ili kuhakikisha mambo hayo hayatokei," alisema.

Sangai aliongeza kuwa ni muhimu vyama vya siasa vikatoa muda sawa kati ya wanaume na wanawake wakati wa kunadi sera, sambamba na vyombo vya ulinzi na usalama kuwapo maeneo yote yanayofanyika mikutano ya kisiasa ili kuimarisha ulinzi bila kujali aina ya vyama.

"Uwapo wa vyombo vya ulinzi na usalama kwenye maeneo yote zinapofanyika kampeni itasaidia wanawake kujiamini na kumwaga sera zao kwa wapiga kura, kwa sababu asilimia kubwa ya wanawake hao hawana uwezo wa kuajiri walinzi binafsi," alisema.

Tayari kampeni za uchaguzi wa serikali za mitaa kwa mwaka huu zilianza jana na kushuhudia viongozi wakuu wa vyama tofauti wakizindua rasmi kwenye mikoa mbalimbali nchini.

## Bisigye afikishwa mahakama ya kijeshi

**KAMPALA, Uganda**

KIONGOZI wa upinzani Uganda, Kizza Besigye amefikishwa katika mahakama ya kijeshi siku moja baada ya kutekwa nyara akiwa Kenya.

Wanachama wa Chama cha Forum for Democratic Change (FDC) ambacho anakiongoza walikusanyika nje ya mahakama hiyo, wakisubiri kuanza kwa kesi ya kiongozi huyo.

Gazeti la Monitor limeripoti kwamba Besogye ambaye ni mkongwe katika siasa, aliripotiwa kutoweka mwishoni mwa juma katika mji mkuu wa Kenya, Nairobi alikokuwa ameenda kwa shughuli binafsi.

Jana, vyanzo vilisema Dk. Besigye, mmoja wa wanasiasa wanaongoza kukamatwa mara nyingi alirejeshwa nchini humo na kushikiliwa katika kambi ya kijeshi ya Makindye kwa ajili ya kufikishwa mahakamani jana.

Kutoweka kwa Besigye kulifuatia kukamatwa kwa wanaharakati 36 wa Uganda wanaohusishwa naye katika mji wa Kisumu.

Wanaharakati hao wa kisiasa walitekwa nyara na kusafirishwa hadi Uganda ambako walifunguliwa mashtaka ya uhaini na kupelekwa katika Gereza la Kitalya.

**BBC**

## Trump amteua waziri wa elimu

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS mteule wa Marekani, Donald Trump amemteua mwanzilishi mwenza wa michezo ya mieleka ya World Wrestling Entertainment (WWE), Linda McMahon, kushika nafasi ya waziri wa elimu.

McMahon, ambaye ni mshirika wa muda mrefu wa Trump, aliongoza shirika la masuala ya biashara ndogo wakati wa uongozi wa kwanza wa Trump.

Trump alitangaza uteuzi wa McMahon kupitia mtandao wake wa Truth, akimwelezea kama mtu mzoefu wa miaka mingi.

„Atatumia uzoefu wake wa miongo kadhaa ya uongozi, na uelewa wake wa kina wa Elimu na Biashara, ili kukiboresha kizazi kijacho cha wanafunzi wa Marekani na wafanyakazi, na kuifanya Marekani kuwa nambari moja katika elimu duniani." Alisema Trump katika ujumbe wake.

Uteuzi wake unakuja saa chache baada ya Trump kumnadi Mehmet Oz, daktari na mtangazaji wa zamani wa televisheni, kuendesha programu mpya ya bima kwa watu wa kipato cha chini iitwayo Medicaid.

Uteuzi wa wawili hao uliofanyika jana uliambatana na ule wa Howard Lutnick kuwa waziri wa biashara.

**BBC**

## Ahoua kinara mabao mguu wa kulia Bara

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Simba, Jean Charles Ahoua na straika wa Fountain Gate, Selemani Mwalimu, wanaongoza kwa kufunga mabao kwa kutumia mguu wa kulia katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara hadi kufikia raundi ya 10.

Kwa mujibu wa takwimu za dawati la michezo Nipashe na za Bodi ya Ligi zilizotolewa jana, wachezaji wao wamefunga mabao matano kwa kutumia mguu wa kulia.

Mchanganuo wa mabao hayo Mwalimu ambaye anaongoza kwenye orodha ya wafungaji Ligi Kuu akiwa amepachika mabao sita, matano aliyefunga kwa mguu wa kulia na moja akitumia mguu wa kushoto, huku Ahoua, raia wa Ivory Coast, anayeshika nafasi ya pili katika orodha ya wafungaji kwa mabao matano, yote ameyapachika kwa mguu wa kulia.

Ahoua amefunga mabao yote matano kwa mguu wa kulia katika mechi ambazo Simba ilicheza dhidi ya Fountain Gate ikishinda mabao 4-0, ambapo alifunga moja, akipachika bao pekee la mkwaju wa penalti dhidi ya Dodoma Jiji, Simba ikishinda bao 1-0, akipachika tena bao moja katika mchezo dhidi Namungo kwenye ushindi wa mabao 3-0, na akafunga mengine mawili dhidi ya KMC, akiiongoza timu yake kushinda mabao 4-0.

Kwa upande wa Mwalimu, mabao yake aliyopafunga kwa mguu wa kulia, ni katika mechi dhidi ya Namungo, timu yake ikishinda magoli 2-0, Dodoma Jiji zikitoka sare ya mabao 2-2, Kagera Sugar akiiongoza timu yake kushinda mabao 3-1, dhidi ya Prisons, ikipoteza mabao 3-2 na KMC, Fountain Gate ikishinda mabao 3-1.

Bao moja alilolifunga kwa mguu wa kushoto lilikuwa katika mchezo dhidi ya KenGold, timu yake ya Simba ikishinda mabao 2-1.

Wachezaji wanaofuatia ni wale waliofunga mabao matatu kwa mguu wa kulia, nao ni Edgar William na Salum Kihimbwa, wote wa Fountain Gate, Paul Peter wa Dodoma Jiji na Marouf Tchakei anayeichezea Singida Black Stars.

Simba yenye pointi 25 ndio vinara wa ligi hiyo yenye timu 16 wakifuatiwa na mabingwa watetezi, Yanga yenye pointi 24 wakati Singida Black Stars ikifuatiwa na pointi zake 23 huku nafasi ya nne ikishikwa na Azam FC yenye pointi 21.

Ligi hiyo itaendelea kesho kwa Pamba Jiji kuwakaribisha Simba wakati keshokutwa Namungo itawafuata Mashujaa na KenGold ikiwaalika Coastal Union kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya.

# COASTAL UNION YAIFUATA KENGOLD KWA TAHADHARI

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Coastal Union kimeondoka jijini Tanga jana kuelekea Mbeya kuikabili KenGold kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Sokoine, huku viongozi wa timu hiyo wakisema watashuka dimbani kwa tahadhari.

Ofisa Habari wa Coastal Union, Abbas El Sabri, aliliambia gazeti hili wanaenda huku wakiwaheshimu wapinzani wao licha ya kutokuwa na matokeo mazuri kwenye michezo yao iliyotangulia.

Sabri alisema wanajua watakutana na timu iliyojiimarisha kupitia mapumziko ya Kalenda ya Kimataifa, kwa kuingia uwanjani wakiwa wamejipanga ni kupata pointi tatu kutoka kwao.

„Tunakwenda Mbeya kucheza na KenGold, pamoja hawafanyi vizuri lakini tunajua haitakuwa mechi rahisi, wao wanahitaji zaidi pointi tatu mara nyingi zaidi kuliko sisi.

Lakini na sisi tumejipanga kushinda mechi hiyo, ndiyo maana nasema utakuwa mchezo mgumu kwa pande zote mbili, kwa maana hiyo lazima twende kwa tahadhari na tucheze mechi kwa uangalifu," alisema Sabri.

Aliongeza katika kipindi cha mapumziko, Kocha Mkuu, Juma Mwambusi, amepata nafasi ya kukaa na kikosi kwa muda wa kuridhisha, akirekebisha maeneo kadhaa yaliyoonekana yana mapungufu hasa kwenye upande wa ushambuliaji.

„Kama mnavyojua Mwambusi ameikuta Coastal katika ligi, kwa hiyo mapumziko haya ameyatumia vizuri sana kuitengeneza timu hasa upande wa ushambuliaji kwa sababu tumekuwa tukitengeneza nafasi lakini zimekuwa hazitumiki vyema, ameonekana kulirekebisha suala hilo ili timu ifunge mabao mengi zaidi," Sabri alisema.

Ofisa huyo alisema wanakwenda Mbeya wakiwa wametoka kucheza mechi mbalimbali za kirafiki na uamuzi huo umelisaidia benchi la ufundi kupata ‚picha' ya uimara kwa kikosi.

Coastal Union inashika nafasi ya 10 katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwa na pointi 12 wakati KenGold inaburuza mkia ikiwa na pointi tano kibindoni baada ya kucheza michezo 11 mpaka sasa.

Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajia kuendelea tena kuanzia kesho kwa vinara, Simba kukutana na wenyeji Pamba Jiji FC kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.



Mashabiki wa Timu ya Soka ya Tanzania (Taifa Stars), wakishangilia baada ya timu hiyo kufuzu tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025). Stars ilipata tiketi hiyo baada ya kuifunga Guinea bao 1-0 na kumaliza katika nafasi ya pili kwenye Kundi H. **PICHA: TFF**

# Mashujaa wafurahia kambi Dar

**Na Mwandishi Wetu**

WACHEZAJI wa Mashujaa FC wamesema wanafurahishwa mazingira ya kambi yao iliyowekwa jijini Dar es Salaam wakitamba imewasaidia kuwaweka imara na kurudisha nguvu tayari kuendelea na michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Katika Kalenda ya FIFA, Mashujaa iliamua kujichimbia jijini na sasa wako tayari kwa mechi ya keshokutwa dhidi ya Namungo FC.

Wachezaji na gazeti hili kwa nyakati tofauti walisema kambi yao ilikuwa na utulivu na pia walipata maeneo bora ya kufanyia mazoezi.

„Tumepata mazoezi mazuri, kwa sababu kuna vifaa bora na maeneo mazuri ya kufanyia mazoezi, pia tulikuwa tumetulia sehemu moja bila kusafiri kwa sababu ligi ilikuwa imesimama, kusema kweli tumerudisha nguvu," alisema straika wa timu hiyo Seif Karihe.

Crispin Ngushi, alisema pamoja na kupoteza michezo miwili ya mwisho kabla ya mapumziko hayo, makocha wamefanya kazi kubwa ya kuangalia mapungufu na sasa wanakwenda kurekebisha kwa kupata ushindi watakapokutana na Namungo.

„Ukiangalia hata mechi mbili za mwisho tulizopoteza siyo kama hatukucheza vizuri, matokeo hayakuwa mazuri tu upande wetu na hilo katika soka huwa linatokea sana," alisema mchezaji mwingine wa timu hiyo, Nassor Idd.

Timu hiyo inashika nafasi ya nane katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 13 na mechi yake dhidi ya Namungo itachezwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani, Kigoma.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LIVER KUMUUZA BECKER

KOCHA wa Liverpool, Arne Slot, yuko tayari kumuuza mlinda lango wa Brazil, Alisson Becker, mwenye umri wa miaka 31 na Caoimhin Kelleher (25), msimu ujao wakati mchezaji wa Valencia na Timu ya Taifa ya Georgia, Giorgi Mamadashvili (24), atakapojiunga na klabu hiyo. ***(TBR)***

### ISAK ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL imemfanya mshambuliaji wa Newcastle United na Sweden, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 25, kuwa kipaumbele chao cha usajili huku Magpies hao wakimtaka Dominic Calvert-Lewin (27) kutoka Everton na Jonathan David (24), wa Lille na Canada kama mbadala. ***(TeamTalk)***

### GULER ANUKIA ARSENAL

KLABU ya Arsenal pia inamwania winga wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Uturuki, Arda Guler, mwenye umri wa miaka 19. ***(Sport)***

### THURAM KUTUA LIVER

LIVERPOOL imefufua mpango wa kumnunua mshambuliaji wa Inter Milan na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Marcus Thuram, mwenye umri wa miaka 27, ambaye ana kipengele cha kuachiliwa cha pauni milioni 70. ***(Gazzetta dello Sport)***

### MARMOUSH KURITHI SALAH

LIVERPOOL pia imeonyesha nia ya kumsajili winga wa Timu ya Taifa ya Misri na klabu ya Eintracht Frankfurt, Omar Marmoush, mwenye umri wa miaka 25, kama mbadala wa Mohamed Salah. ***(Give me Sport)***

### ALONSO KUIJIBU MADRID

KOCHA wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso mwenye, umri wa miaka 42, ambaye anawaniwa na Real Madrid, atafanya uamuzi kuhusu hatima yake ifikapo Machi mwakani. ***(Marca)***

### DRAGUSIN HAUZWI JANUARI

WAKALA wa mchezaji wa Tottenham Hotspur, Radu Dragusin, mwenye umri wa miaka 22, amefuta uwezekano wa uhamisho wa mkopo wa beki huyo wa Romania katika dirisha la Januari, lakini amedokeza kuhusu uhamisho wa majira ya joto. ***(Tuttomercato)***

### SON ATAJWA UTURUKI

KLABU ya Galatasaray imeonyesha nia ya kumsajili nahodha wa Tottenham Hotspur na Korea Kusini, Son Heung-min, mwenye umri wa miaka 32, ambaye mkataba wake na klabu hiyo ya Ligi Kuu England unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Fanatic)***

### LLORENTE KUTUA VILLA

KIPAUMBELE cha Aston Villa dirisha la usajili wa wachezaji litakapofunguliwa Januari kitakuwa kupata beki mpya, huku kiungo wa Real Betis, Diego Llorente, mwenye umri wa miaka 31, akiwa kwenye orodha yao. ***(Football Insider)***

### LUKEBA ATAKIWA CITY

MANCHESTER City inatathmini uwezekano wa kumnunua mlinzi wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Castello Lukeba, mwenye umri wa miaka 21, huku wakijiandaa kuimarisha safu yao ya ulinzi. ***(Football transfers)***

### NEWCASTLE, CHELSEA VITANI

KLABU ya Newcastle United inatazamia kumnunua winga wa Sporting na Timu ya Taifa ya Ureno, Geovany Quenda, mwenye umri wa miaka 17, lakini inakabiliwa na ushindani kutoka kwa Manchester United na Chelsea. ***(Give Me Sport)***

## DO… O ZA SOKA MA… TI YA ULAYA




# BARCA: TULIWAKATALIA PSG KUMSAJILI YAMAL

### Licha ya vigogo hao wa Ufaransa kuweka dau nono ili kuziba pengo...

**BARCELONA, Hispania**

OFISA wa Barcelona, Enric Masip, amesema Paris Saint-Germain ndio klabu ambayo ilitoa ofa ya euro milioni 250 kwa ajili ya kumnunua mshambuliaji chipukizi, Lamine Yamal, msimu uliopita wa joto.

Mwezi uliopita, Rais wa Barca, Joan Laporta, alifichua viongozi hao wa LaLiga walikataa ofa hiyo kubwa ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17, lakini hakuthibitisha ni wapi ofa hiyo ilitoka.

"Rais tayari amesema kulikuwa na ofa yenye thamani ya euro milioni 250 ambayo ilikataliwa na haikuzingatiwa hata kidogo," alisema Masip, ambaye ni sehemu ya tume ya michezo ya klabu na mshauri wa Laporta, akiiambia El Chiringuito.

PSG ilimpoteza fowadi wao Kylian Mbappé aliyetumkia Real Madrid msimu uliopita wa joto, jambo ambalo lilimaanisha walikuwa wakihaha kutafuta mbadala wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa.

Alipoulizwa kama PSG ndio klabu inayozungumziwa na kama Yamal angekuwa mbadala mzuri wa Mbappé, Masip aliongeza: "Unapokuwa na fedha za kutumia, unaweza kutamani kujaribu kumsajili yeyote unayemtaka."

Ujio wa Mbappé nchini Hispania ulipaswa kuipeleka Madrid kwenye kiwango cha juu zaidi, lakini mashambulizi ya mabingwa hao wa LaLiga na Ligi ya mabingwa Ulaya yamezidiwa na wachezaji watatu wa Barca, Yamal, Raphinha na Robert Lewandowski.

Yamal amefunga mabao sita na kutengeneza mengine nane katika mechi 16 katika michuano yote, huku Barca akipoteza michezo miwili pekee ya ligi hadi sasa.

"Ningesema kwa sasa yeye ndiye mchezaji mwenye maamuzi zaidi duniani," alisema Masip alipoulizwa kama Yamal kwa sasa ndiye bora zaidi duniani.

"Sidhani kama ni vizuri kuzungumza juu ya mtoto wa miaka 17 kuwa bora zaidi ulimwenguni, lakini kwetu yuko."

Yamal alikosa mchezo wa mwisho wa Barca kabla ya mapumziko ya kimataifa wakati wakichezea kichapo kutoka kwa Real Sociedad.

# Amorim hatapewa bajeti ya kusajili

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United imemtaka Rúben Amorim kutengeneza ubora zaidi kwenye kikosi alichorithi hapo Old Trafford badala ya kutegemea kusajili wachezaji wapya, kwa mujibu wa ESPN.

Amorim amewasili kama kocha mkuu na anatarajiwa kuchukua jukumu la mchezo wake wa kwanza dhidi ya Ipswich Town utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Portman.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 39, ambaye amesaini mkataba wa miaka miwili na nusu, amepewa jukumu la kupata zaidi ubora kutoka kwenye kikosi hicho kilichopo nafasi ya 13 katika msimamo wa Ligi Kuu England.

Chanzo kiliiambia ESPN wasiwasi wa kifedha katika klabu unamaanisha hakuna uwezekano wa kupata bajeti kubwa ya usajili wakati wa dirisha dogo la Januari.

Ingawa kazi ya kusajili United sasa inaendeshwa na Mkurugenzi wa Michezo, Dan Ashworth, na Mkurugenzi wa Ufundi, Jason Wilcox, chini ya muundo mpya wa INEOS, Amorim atakuwa na usemi katika wachezaji watakaosajili.

Lakini chanzo kiliiambia ESPN bajeti ya usajili nu ngumu kwa sasa katika kikosi hicho.

Mtangulizi wa Amorim, Erik ten Hag, alitumia muda mwingi katika soko la uhamisho, akisajili wachezaji 15 wa kikosi cha kwanza kwa gharama ya zaidi ya pauni milioni 600.

Chanzo kimoja kiliiambia ESPN, idadi hiyo haiwezi kulinganishwa kwa miaka mitatu ijayo na kazi ya Amorim itakuwa kuboresha uchezaji na kikosi kilichopo.

Bosi huyo wa zamani wa Sporting CP anatazamiwa kutekeleza mtindo mpya wa kimbinu akiwa United, akitumia mfumo wa 3-4-3 ambao ulionekana kuwa na mafanikio nchini Ureno.

# Vieira kocha mpya Genoa

**ROME, Italia**



KIUNGO wa kati wa zamani wa Arsenal, Patrick Vieira, yuko mbioni kurejea kwenye uongozi wa klabu akiwa anatajwa atapewa mikoba ya kuinoa Genoa inayoshiriki Ligi Kuu Italia, Serie A.

Mfaransa huyo aliisimamia kwa msimu mmoja tu klabu ya Strasbourg, kabla ya kuondolewa majukumu yake wakati wa maandalizi ya msimu mpya.

Sasa akiwa katika harakati za kutafuta kazi ya tano ya uongozi mkuu katika maisha yake ya soka, Vieira anatarajiwa kutua Genoa, huku Fabrizio Romano akifichua kuna makubaliano tayari kwa kocha huyo mwenye umri wa miaka 48 kuchukua jukumu hilo.

Genoa ilitangaza kuachana na Alberto Gilardino tangu Jumanne iliyopita na wanatarajiwa kumtangaza Vieira kama mbadala wake mara moja.

Kuhamia Genoa, ambayo iko katika nafasi ya 17 kwenye msimamo wa Serie A, kutamfanya Vieira kuungana na mchezaji mwenzake wa zamani wa Manchester City, Mario Balotelli, ambaye alijiunga na Genoa majira ya joto na bado anasubiri bao lake la kwanza.

Maisha ya ukocha ya Vieira yalianzia Manchester City, akifanya kazi katika akademi kabla ya kuinoa New York City FC, lakini hapo awali aliacha milango wazi ya kurejea Arsenal.



# GUARDIOLA AONGEZA MWAKA MMOJA CITY

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amekubali kusaini mkataba mpya wa mwaka mmoja ili kuongeza muda wake wa kubakia Manchester City, kwa mujibu wa ESPN.

Mkataba wa sasa wa Guardiola unaendelea hadi mwisho wa msimu huu na kocha huyo mwenye umri wa miaka 53 bado hajazungumza juu ya mipango yake.

Lakini baada ya mazungumzo mazuri kati ya Guardiola na mabosi wa klabu hiyo, kocha huyo wa zamani wa Barcelona anatazamiwa kubakia kwenye Uwanja wa Etihad kwa msimu wa 10.

Guardiola tayari ndiye kocha aliyefanikiwa zaidi katika historia ya klabu hiyo, akiwa ameshinda mataji 15 makubwa, yakiwamo sita ya Ligi Kuu England, tangu awasili kutoka Bayern Munich mwaka, 2016.

Vyanzo viliiambia ESPN, Guardiola alitarajiwa kufanya uamuzi kuhusu kusaini nyongeza wakati wa mapumziko ya kimataifa.

Nyongeza zake mbili zilizopita, mnamo 2020 na mwaka 2022, zilitiwa saini Novemba ili kuzuia uvumi kuhusu mustakabali wake kuenea katika nusu ya pili ya msimu.

City wamepoteza michezo minne iliyopita katika michuano yote, lakini bado wanashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, pointi tano nyuma ya vinara, Liverpool.

Pia wanatazamiwa kushiriki katika michuano ya klabu bingwa ya Dunia itakayofanyika nchini Marekani ifikapo Juni, mwakani.

# FADLU AKABIDHI FAILI USAJILI DIRISHA DOGO

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI dirisha dogo la usajili likikaribia, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, tayari amepenyeza faili la usajili akitaja maeneo anayotaka yaongezewe nguvu kwa ajili ya kufanya vizuri katika Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa wanayoshiriki, imefahamika.

Taarifa za ndani zimesema Fadlu ameweka wazi maeneo ambayo yanatakiwa kuboreshwa.

Akizungumza na Nipashe juzi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, kabla ya mchezo wa kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Kombe la Mataifa Afrika (AFCON 2025), kati ya Tanzania dhidi ya Guinea, mmoja wa viongozi wa klabu hiyo alisema baada ya dirisha dogo la usajili kufunguliwa pia kutakuwa na wachezaji watakaoachwa.

"Tayari kuna baadhi ya majina Fadlu amependekeza kusajiliwa, ametoa wasifu wa wachezaji hao, kazi imebaki kwa viongozi kumalizana nao ili Januari wawe sehemu ya kikosi chetu, lengo ni kuimarisha timu zaidi," alisema kiongozi huyo ambaye hakutaka jina lake litajwe.

Aliongeza kwa sasa viongozi wanaanza mchakato wa kuzungumza na wachezaji hao ambao hata hivyo kiongozi huyo hakutaka kutaja majina yao.

"Muda ukifika mtawajua, lakini kocha ametaka kusajiliwa kiungo wa juu (kiungo mshambuliaji), beki wa kati na winga, tayari viongozi wameanza kufanyia kazi mapendekezo hayo, kwa sababu tunataka kuzidi kukijenga kikosi chetu," alisema kiongozi huyo.


Aliongeza kwa nafasi ya winga, kocha huyo ameridhishwa na uwezo wa Elie Mpanzu ambaye tayari ameanza mazoezi na timu hiyo ana atakuwa sehemu ya kikosi baada ya dirisha dogo kufunguliwa.

"Maeneo yaliyobaki ni kiungo kama nilivyosema na beki mmoja wa kati, hii Simba itakuwa tishio sana nawaambia, tusubiri muda utaongea," alisema kiongozi huo.

Wakati huo huo, Fadlu alikuwa ni sehemu ya viongozi na mashabiki walioshuhudia mechi kati ya Taifa Stars dhidi ya Guinea, ambayo ilimalizika kwa wenyeji kupata ushindi wa bao 1-0.

Katika mechi hiyo Fadlu amewatazama wachezaji wake watano waliokuwa sehemu ya vikosi vya timu hizo mbili katika mchezo huo wa mwisho wa hatua ya makundi.

Nyota hao ni pamoja na Aishi Manula, Shomari Kapombe, Mohamed Hussein na Kibu Denis waliopeperusha bendera ya Stars huku pia Guinea kulikuwa na kipa, Moussa Camara.




Kipa wa Timu ya Soka ya Tanzania (Taifa Stars), Aishi Manula (kulia), akiwa na kocha wa makipa wa timu hiyo, Juma Kaseja (katikati), baada ya mchezo wa kufuzu fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025), dhidi ya Guinea. Kushoto ni kipa namba tatu wa Stars, Zuberi Foba. **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**

# Msuva: Nitamfikia Ngasa Morocco

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya kufunga bao pekee lililoipeleka Tanzania katika Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025), zitakazofanyika mwakani nchini Morocco, na kufikisha idadi ya mabao 24 kuifungia timu hiyo, winga, Simon Msuva, amesema ataifikia rekodi ya kupachika mabao mengi kwa taifa lake.

Bao hilo lililofungwa na Msuva juzi lilifanya afikishe mabao 24, moja nyuma ya kinara, Mrisho Ngasa.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Msuva alisema kwa msaada wa Mungu anaweza akaifikia rekodi ya Ngasa kama atakuwa sehemu ya kikosi cha Stars kitakachoshiriki fainali hizo.

"Kwanza namshukuru Mungu kutuwezesha kufuzu AFCON, cha kwanza ilikuwa kufuzu kabla ya kuangalia rekodi binafsi, naamini kwenye fainali zijazo naweza kufikia rekodi ya kaka yangu Ngasa," alisema Msuva.

Alisema ushindi walioupata ni kwa ajili ya watanzania wote lakini rasmi anaupeleka kwa walioathirika na ajali ya kuporomoka ya ghorofa yalitokea Kariakoo hapa jijini.

"Ushindi huu ni kwa ajili yao, kwa pamoja tunahuzunika na kile kilichotokea kwa wenzetu Kariakoo, natoa pole lakini goli nililofunga nalitoa kwa ajili yao," alisema Msuva.

Nahodha wa timu hiyo, Mbwana Samatta, anashika nafasi ya tatu akiwa na mabao 22.

## Serikali: Asante Taifa Stars

INATOKA UK. 24

nashukuru mchango wa rais huyo ambao ameutoa kwa Stars kuanzia huko nyuma hadi walipofanikiwa kufuzu fainali hizo kwa mara ya nne.

"Kwa niaba ya wachezaji, zawadi ambayo imetoka kwa mama, tunafahamu ni kipindi kipindi ambacho nchi inapitia, na yeye kama mama yetu, ni kipindi kigumu anapitia, tunamshukuru kwa zawadi hii, tunamshukuru kwa yote aliyoyafanya, tunamshukuru sana mama, tunajua unatuangalia, tunakuongeza kwa Mungu, aendelee kukupa afya na kuendelea kutujali na wengine wote unaowajali hapa Tanzania," Samatta alisema.

Jamhuri Julio, ambaye pia yuko katika benchi la ufundi la Stars, alisema umefika wakati makocha wazawa wakaaminiwa kwa sababu wana uwezo na uzoefu wa kuzipa mafanikio timu zetu.

Julio alisema anaamini Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), na wadau wengine wakiwaamini makocha kutoka hapa nchini, mafanikio yatapatikana na nchi inafika mbali.

"Umefika wakati makocha wazawa tukaaminiwa, uwezo na uzoefu tunao, ninawapongeza sana Morocco na Mgunda (Juma), kwa mafanikio haya, tuwape nafasi, hakuna ambacho makocha wakigeni wanacho na sisi makocha wazawa hatuna," Julio aliongeza.

Taifa Stars inaungana na Uganda (Uganda Cranes) na Sudan ambazo zimetoka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), kufuzu kushiriki fainali hizo.

## Ramovic wa Yanga awavuruga Al Hilal

INATOKA UK. 24

kucheza na timu kubwa sana kwa sasa Afrika, hivyo itakuwa ngumu sana kwetu, inatakiwa kuandaa mikakati ya kumsoma angalau kwa uchache kocha mpya," aliongeza kocha huyo.

Mechi ya Yanga dhidi ya Al Hihal itachezwa Novemba 26, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na mechi hiyo itakuwa ya kwanza kwa Ramovic.

Mjerumani hiyo anakabiliwa na kibarua cha kuendeleza mafanikio yaliyoachwa na Gamondi ambaye licha ya kuiwezesha timu hiyo kutinga hatua ya makundi msimu huu baada ya mara ya mwisho vigogo hao kucheza hatua hiyo ilikuwa ni mwaka 1998.

Kikosi cha Gamondi kilitolewa kwa mbinde na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini kwa penalti 3-2, mechi iliyochezwa Aprili 5, mwaka huu baada ya kutoka suluhu michezo yote miwili, mechi ya kwanza ikifanyika Machi 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Michezo
Alhamisi Novemba 21, 2024
Nipashe

## Guardiola aongeza mwaka mmoja City

UKURASA 22



# SERIKALI: ASANTE TAIFA STARS

●●●Yaridhishwa na kiwango cha timu hiyo, kuanza mapema maandalizi ya...

**Na Faustine Feliciane**



Winga wa Timu ya Soka ya Tanzania (Taifa Stars), Simon Msuva (kulia), akijiandaa kumtoka beki wa Guinea, Issiaga Sylla (kushoto), katika mechi ya Kundi H ya kusaka tiketi ya kufuzu Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025), iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. Stars ilishinda bao 1-0. **PICHA: TFF**

HUKU Rais Samia Suluhu Hassan akitoa motisha ya Sh. milioni 700 kwa wachezaji wa Timu ya Soka ya Tanzania (Taifa Stars), kufuatia kufuzu tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (AFCON 2025), ni, Serikali imesema imeridhishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wa timu hiyo kwa kupambana hadi kufikia malengo ya nchi.

Ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Guinea, umeifanya Taifa Stars kufikisha pointi 10 na kumaliza katika nafasi ya pili kwenye Kundi H nyuma vinara Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo), iliyomaliza na pointi 12 kibindoni.

Akizungumza baada ya mchezo huo kumalizika, Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma 'Mwana FA', alisema kilichoonyeshwa na wachezaji wa Stars ni kuipambania bendera ya taifa katika mechi zote za hatua ya makundi.

Mwana FA alisema mara baada ya mechi dhidi ya Ethiopia ambayo alikuwa sehemu ya msafara wa timu hiyo, juzi wachezaji walionyesha zaidi kiu ya kutaka kushiriki fainali hizo zitakazofanyika mwakani nchini Morocco.

"Bahati nzuri hata mchezo wa Guinea na DR Congo bado tulikuwepo Congo, baada ya mchezo ule wachezaji wa Guinea walishangilia sana kuwafunga Congo, nilikuwa na wachezaji wa Stars wakaniambia waache washangilie sisi tutaenda kumalizana nao kwa Mkapa, na kweli leo (juzi), wachezaji wameonyesha kile walichoniambia, wamepambana na Guinea amekufa hapa kwa Mkapa," alisema Mwana FA.

Naibu Waziri huyo alisema Serikali imeridhishwa na juhudi na kujituma kwa wachezaji hao wakati wote na kuwapongeza kutokana na kuthamini mchango wao.

"Tunaenda kujipanga sasa kwa ajili ya kuhakikisha timu inakuwa na maandalizi mazuri kuelekea katika fainali hizo zitakazofanyika Morocco, tumefarijika sana," alisema kiongozi huyo.

Naye Kaimu Kocha Mkuu wa Stars, Hemed Suleiman 'Morocco', aliliambia gazeti hili amefurahi kuwa sehemu ya historia ya soka la Tanzania kwa kuiwezesha Taifa Stars kufuzu kwa mara ya nne kucheza fainali za AFCON.

"Najua hatukupewa nafasi kubwa ya kufuzu, lakini nilijua nafasi ipo kama tutapambana na kuchanga karata zetu vizuri, najivunia matokeo haya na kuwa sehemu ya historia ya soka la Tanzania," alisema Morocco.

Aliongeza pia anawashukuru sana wachezaji wake kwa kupambana na kufanikiwa kufuzu fainali hizo.

Nahodha wa timu hiyo, Mbwana Samatta, alisema anamshukuru Rais Samia kwa zawadi aliyowapatia na anamshukuru kwa nguvu kubwa anayotumia katika kuendeleza michezo nchini.

Samatta aliongeza wa-

INAENDELEA UK. 23

## Ramovic wa Yanga awavuruga Al Hilal

**Na Adam Fungamwango**

MABADILIKO katika benchi la ufundi la Yanga, yameonekana 'kumtisha', Kocha Mkuu wa Al Hilal Omdurman ya Sudan, Florent Ibenge, ambaye amesema yeye alijiandaa kupambana na aliyekuwa Kocha Mkuu, Miguel Gamondi na si Mjerumani, Sead Ramovic

Yanga ilitangaza kuchana na Gamondi wiki iliyopita na Ramovic kutoka TS Galaxy ya Afrika Kusini alikabidhiwa mikoba ya kuwaongoza mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza jijini Dar es Salaam baada ya kuwasili kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa hatua ya makundi wa mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Ibenge, alisema maandalizi waliyokuwa wameyafanya awali ni kwa ajili ya kukabiliana na mfumo unaoongozwa na Gamondi.

Ibenge alisema kwa nyakati mbalimbali alikuwa 'ameshamsoma' na kujua mbinu za Gamondi na kukiandaa kikosi chake kukabiliana na ushindani huo, lakini ujio na Ramovic, umemchanganya.

"Tulishamjua aina yake ya uchezaji na mifumo ya Gamondi, tulifanyia kazi namna timu yake inavyocheza, huyu mpya kwetu itakuwa ni mgumu sana, hatujui lolote, hatujui atakuja na mbinu gani. Tunatakiwa kuwa makini sana," alisema Ibenge.

Mkongomani huyo alisema kundi lao lenye timu za Yanga, Al Hilal, MC Alger ya Algeria na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo), ni gumu na kila timu ina uwezo wa kuifunga timu nyingine na kutinga hatua ya robo fainali.

"Kila timu inataka kwenda robo fainali na kundi letu (Kundi A), timu yeyote inaweza kumfunga mpinzani, zina uzani na ubora unaolingana, hivyo tunatakiwa tupate pointi nyingi kwa kadri inavyowezekana," alisema Ibenge.

Aliongeza kwa sababu hiyo aliamua kuwasili nchini mapema kwa ajili ya kukamilisha maandalizi ya mchezo huo ambayo ni pamoja na kuzoea hali ya hewa ya Dar es Salaam ambalo kwa sasa joto.

"Ni mechi kubwa sana kwetu, tunatakiwa kujitayarisha vizuri na umakini zaidi na ndiyo maana tumekuja mapema, unajua tunakwenda

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >